Translator : Mama pia anapendekeza kuwe na court, mahakama area kama hii ya Garbatula.

Mama Balafu Gabo : *Yoo aarr nyyonggan jeedaanii, taa khaalee nuu kootiini issaa cuuf woolin khee jiirree llaalee birraa yaan feen*

Translator : Anasema kama mtu akipelekwa kwa court, huwa saa ingine anasikia mtu ana hukumiwa kunyongwa, na... lakini akiwa hiyo court iko area hii, pia wale jamaa zake wakiwa wameshitakiwa wanaweza kwenda kusikiza hiyo court, ikiwa haina shida kwao kwa sababu ya court kuwa mbali.

Mama Balafu Gabo : *Nuu aammalee nuu siirkaal akhaa maalee woolt aann feen khaa siirkaali nuut ann*

Translator : Mama pia anapendekeza ya kwamba uhusiano wetu jamii ya huku na ya Serikali iimarishe we iwe mzuri zaidi ya sasa.

Mama Balafu Gabo : *Nuu aammalee sheerriyya teen taa issilaanaa, hoojja saafaari khaaraa deemnuulee nuu fuulaa waaktiin teen ittii geet cuufaa raabbiudhaa kaadaanaa, kaanissa jeenee irraingooru, waakti suun naamicii dheerevalee khaa gaarri nuu daabee saalaadhii nuu kuubbaalutii*

Translator : Anasema sisi huwa tukiwa hata safarini huwa wakati wa sala ikifika, tungependa kusimama mahali kusali na hata kwa wale jamii zetu... wengine majirani yetu wale tuko nao hata madereva. Tunataka tuheshimiwe katika kuwa na hiyo nia ya kutaka kusa... kusali, kuomba, kwa sababu hiyo ni sheria yetu ni lazima tuifuate.

Mama Balafu Gabo : *Nuu ammaalee, nuu woorri jiirrankii teena siirkaali kheen khaa keenyaaleeni naadeen woorri guuracalee shaambaa qootitii dhaabbaartee, nuulen tissitii dhaabaarre khaamuu shaambaa, niitii shaambaa maajaani irraa guurt biic和平 daanii TV khee gaarssissanii, nuu niitii loon eellmituuyu akh nuu loon eelmin nuu gaarsissu dhiidhaan, siirkaalii kheen khaa keenyaa*

Translator : Mama anasema sisi pamoja na majirani zetu kila moja ana kazi yake maalum. Kwa mfano anasema majirani zetu wa upande wa down... Meru. Mama anaenda shamba kulima. Mama ya huku kwetu anaenda kuchunga na kukamua ng'ombe. Anasema anaona kila wakati, huyu mama kwa shamba ya majani ya chai, huwa anapigwa picha anakuwa advertised. Ana onekana. Anajulikana, anakuwa recognized. Ile kazi anafanya. Anasema

sisi kwetu hata siku moja hatuja ona hata picha ya Mama moja ameonekana akiwa anakamua ng'ombe as a form of advertisement. As a form of recognition. Anasema anataka sisi pia tuwe recognized tujulikane, tutambuliwe. Kama ni mtu wa shamba, ni kazi ya shamba. Na sisi pia ni watu wa mifugo ni kazi ya mifugo. So tutambuliwe katika ile kazi yetu.

Mama Balafu Gabo : *Nuuin ammalee, nuu adhaa teen taa siirkaalaa, aadhaa teen taa booraanaa, booraanii waan jeedee, "naadeen dhuubr daaltee haaqqi inqqaabd jeedee waan waaqqi sii kheen fuudataa muuccaa hiirren intoolfaatuu, niitiin dhuubr daalt daalkii inqaabdh jeetee booraanii akhaassin naamii kheen khaa issiilaanaa, niitii waaqqi intaalluum kheeneef daalkii doowee, aadhaa teen taa issiilaanaa niitiin ijjoolle duubraa daaltee haaqqi inqaabdh jeedee, indaalaan jeedee, woomaa indaal jeedee wooni buushooftuu took dealt jeedee suunuman dhaanaabb aabban hoorraat intaal aabbaan daal haaqqii doowe loon khaan goossat ooffaat jeedanii, naamiccii aabbaa hoommaa itaan loon ooffaatee waan waaqii kheeneef gaarraci aarmmuumat oobbas".*

Translator : Mama anasema katika mila ya Kiborana, mama akizaa mtoto wa kike, mtoto msichana huwa hawezি pata kurithi hata mali ya Baba. Anasema, anataka kupendekeza kwa Katiba ile hapa Kinna, wale wasichana wa yule mama hata kama hakuzaa mwanaume. Kupata mwanaume, kupata msichana pia ni amri ya mwenyezi Mungu. Anasema anataka hata yule msichana apatiwe haki kama vile kijana anapatiwa.

Mama Balafu Gabo : *Haqqii woorr suunii khaa akh taakaa toolcaanitii, illmaan khaamuu rabbi naamaa kheenee, nuu haaqqi issi taa haagg taakaa toolcaan feena*

Translator : Anasema anataka haki ya hawa watoto wasichana na wavulana pia, iwe ni sawa, wapatiwe haki kila moja.

Mama Balafu Gabo : *Diirtii nuu dhaabbsitee aadhoo gaanii kheen shaantaam taatee, hoojjaa nuu taamboo kaadaanaa oollaa khee baan, aakkoon taantee mee jeedee aakhaakhuu woorraa aafaan baanaa deemt jeedee nuu daan guuyya cuuf, uulleen shaantaam gaannalle nuuraa inn [inaudible]*

Com. Muigai : ...[inaudible]... that one we are giving her more time, we are giving her more time, because she is a spokesman..

Translator : Mama anasema ya kwamba kutoka kwa ujana wake, mpaka kufikia miaka za hamsini. Huwa wanaume wana wadhulamu kina mama kwa sababu, hata akitoka kwa jirani, kwenda kuomba kitu kwa jirani mwenzake, huwa akirudi, ana pigwa. Anasema anataka kupendekeza kwa Katiba hiyo sheria ya akina Mama

kupigwa ipigwe marufuku.

Com. Muigai : ...[...ha Ha! ha...]. . .

Com. Lethome : Wazee mbona hampigi makofi?

Com. Muigai : ...[...ha Ha! ha...]. . .

Mama Balafu Gabo : *Nuu aammalee booraanii goositii teenaa, intaal fuutee intaal taan aammaarkiin raabbi guudhaa illmaan inkeenineefii gaan dhiidhaamaa daaciiteefii, gan dhiidhaamaa tiisiiteefii woyyaa issaa miiciiteefii, ookootee issaa daabbdheefi, ibbiidhee guubbe, adhuun guubdhee, oommaa indaalee haqqii inqaabbdhuu eedee oojja issin jaartee uuffijibbat khaa woorraa gaaltuu jeedee akhaassi gaalcaan waan cuuf irra fiitaatee,*

Com. Muigai : The women are happy.

Mama Balafu Gabo : *Akhaasifuu dhaabb khaan qaabbnaa dhaabbi kuuun khaa nuurraa buuqaauu feen*

Translator : Anasema katika mila ya Kiborana, ma... ma... mke akiolewa aishi huko kwa bwana awe kwa bahati mbaya, hajapata mtoto. Lakini amemtumikia ule Bwana katika kila hali. Kama ni kuchunga, kama ni kupika, kila kazi amemfanyia. Lakini kama hajapata mtoto huwa yule mama anadhulumiwa. Kwa sababu wakati wa uzee wake anaambiwa, huyu hana maana. Rudisheni yeze kwao.

Sasa anasema anataka wapatiwe haki, kwa sababu kule kupata mtoto ni amri ya mwenyezi Mungu. Sio mapenzi ya yule Mama. Kwa hivyo anasema, amemtumikia, amepigwa na juu, ame chomwa na moto, amepata kila shida katika kutumikia ile family, kwa hivyo anasema wapatie... anapendekeza katika Katiba wapatiwe haki. Hata kama hajapata mtoto. Kule kupata mtoto au kukosa mtoto sio kuchaguwa kwake.

Mama Balafu Gabo : *Aan dhuubbin tiyyaa haagganuumaa naadeen eedhuut eeggee jiirraa dhuuraa infiitaaduu siillaa guuyyaa khaan naaraa inn hoobbatuu, akh dhaabb diirtii nuu dhaabbsitetii tiyy haagganuumaa naaggat.*

Translator : Mama anasema akona... mengi ya kusema lakini kuna akina mama wengi anataka kuwapatia nafasi. Hataki kumaliza mazungumuzo yote na anasema kwa hayo asante.

Com. Muigai : Asante Mama. Halima Ali... Halima Ali...

Com. Muigai : Wale watu wamefika hapa, na hawaja weza kuijandikisha tafadhali mujiandikishe kule, kwa wale vijana pale. Ukipika hapo tafadhali ujiandikishe ukiwa una maoni, au hata ukiwa umekuja ku sikiza. Tafadhali jiandikishe huko.

Translator : *Naammii aarm duuff, issanii aarm jiirtaan khaan naamii maaqaa inqooraatin khuun fuulaa ijollee suunii daaqaa aartii maaqaa qooraadaa, yoo waa caaqaasuu duufteef hoojjaa maaonii taantee baasuu duufteelee maaqqa khee aarti qooraad*

Mama Halima Ali : ...[Arabic]... mimi kwa jina naitwa Halima Ali. Niko na pendekezo langu na mimi naweza kutoa. Napendekeza nataka kutoa kidogo moja mbili hivi. Kama mimi mama pia. Kwa hivyo mimi natoa maoni yangu kuhusu wakina Mama. Kama mimi sasa mjane. Nime fiwa na Bwana yangu ...[Vernacular]... kama mimi Mama mjane hivi nime fiwa na bwana yangu. Na kila siku niko na watoto nawaacha mimi kwenda kutafuta haki wa bwana yangu, sipati. Na sikhenda kutafuta pesa kwa mtu ama kutafuta kwa jamaa. Ni kwa Serikali. Na Serikali inatunyanya.

Unaona watoto wangu wanateseka na mimi, nateseka kila siku ni kuondoka na kwenda. Death Gratuity ni pesa za haki za Mzee wangu marehemu ikiwa yeye ni mfanyi kazi ya Serikali. Kila siku mara niko Uchumi House, ama huko Sheria House, Public Trustees kufuutilia, na hakuna kitu ninapata. Shida ni ile ile. Na si tafuti pesa kwa mtu. Naona kwa hivyo Serikali ina tunyanya sisi, sijui ni sisi tu kina mama peke yake ama ni watu wote, ama ni watu wa dini ya Kiislamu peke yake, ama ni upande yote. Siwezi kutafautisha.

Kwa hivyo naomba Katiba ituangalilie kwa... tunafaa kuangaliliwa pesa zetu wanaume, wanawake waki fiwa pesa... Kwa maana ni haki yake mwenyewe, aletewe nyumbani kwake. Sio wewe unawacha watoto, watoto wanateseka. Huku wewe ukienda, hakuna mtu anakuangalilia watoto. Huku hupati pesa zako na sio haki yako... sio haki yao ati unaenda kuwaomba. Kwa hivyo tunaomba Katiba itusaidie hata hapa. Kwa hivyo ndio maoni yangu ya kwanza.

...[inaudible]...

Ya pili tuko na mahospitali wengine kama sisi hivi tunakaa sehemu za... tuko vijihi hivi... sio town. Hatuna madawa, hatuna matibabu yoyote tunapata. Ikiwa wewe huna pesa. Huwezi kusaidiwa, unaweza kuteseka hapo hapo, ama unaweza kufa hapo. Kama ni mama mjamzito ameletwa anajifungua na ako na maumivu na una juu uchungu wa mzazi. Hapati msaada yoyote kusaidiwa, anga huyu mama ajifunguwe ndio badaye hata matibabu yapatikane. Kama ni pesa zifuatiliwe ama pesa, kutafuta njia ile watalipia, hauwezi. Unaweza kufa hapo hapo na

na nini... na umeletwa hospitali. Unakufa mbele yao. Kwa hivyo pia hapo upande wa hospitali hatuna madawa, tuko na shida kama hizi.

Upande tena wa mifugo, kwa maana sisi ndio watu wa mifugo tuko na mifugo kama ng'ombe, mbuzi na ng'amia. Wakiliwa na wanyama wa pori hatulipwi, unaona. Tuko na shida kama hizo pia. Tunafaa tulipwe kama ni mifugo wengine hawana uwezo wanategemea hiyo mifugo tu. Kwa hivyo wanafaa wapewe, kama ni kulipwa hivi. Wanafaa kulipwa maana mategemeo yao yote ni hiyo mifugo hawana kazi nyengine, pengine ya kufanya. Kuna wengine kweli wanafanya kazi na wako na mifugo. Lakini wengi wao hawana kazi, hawana chochote. Hiyo ndio kazi yao. Mifugo tu, kutegemea mifugo. Kwa hivyo kama ni wa nyama wa pori wamekula mifugo yetu, kwa vile sisi ni wafugaji, tunafaa tulipwe. Yangu ni hayo machache Asanteni.

Com. Muigai : Asante Sana.

Com. Lethome : ...[inaudible]... mwanadamu akiuliwa na mnyama wa pori?

Mama Halima Ali : ... Pia anafaa alipwe, kwa maana kama... kama mifugo yenye tuna faa tulipwe, binadamu si ni bora zaidi.

Com. Lethome : ...[inaudible]... sasa tunasikia kuwa wanalipwa shillingi elfu thelathini binadamu akiuliwa na mnyama wa pori... unapendekeza nini, ikae hivo hivo ama nini?

Mama Halima Ali : Elfu thelathini si pesa za kulipa binadamu.

Com. Lethome : Pendekeza.

Mama Halima Ali : Ina faa tulipwe [?] zaidi ya hapo.

Com. Lethome : Kama elfu... kama millioni moja hivi, ama millioni mbili, ndio zina faa kusaidia hao jama waliofiliwa. Asanteni.

Com. Muigai : Okay. Bwana Hussein Roba.

Mr. Hussein Roba : ...[Arabic]... Basi yangu hayatakuwa mengi, lakini yatakuwa machache. Ya kwanza ili kusindikisha tu yale yameweza kuzungumuzwa na wengine. Ya kwanza, kama tunavyoju, katika nchi yetu tukufu ya Kenya, tuna tawaliwa, au tunalindwa na sheria ambazo zimeundwa na binadamu. Na hii sheria ambazo

zimeundwa na binadamu, huwa inarekebishwa mara kwa mara. Malengo yake huenda yaki teuzi... yasiweze kutimizwa. Kwani kila wakati, tunapata shida, hata katika kuhukumu au kijiendelesha katika dini yetu. Yaani tuna shindwa kukuwa na ku-practice, au kutumia, au kuweza kujilinda katika la... kwa kutokana dini tukufu ya mwenyezi Mungu dini ya Kiislamu, au kutokana na hukumu ya mwenyezi Mungu kutokana na Koran tukufu.

Kwa hivyo katika shughuli hii ambazo zina endelea za kurekebisha Katiba, ningeomba Serikali au wale ambayo wanahusika ku-consider zaidi a Federal system. Federal Islamic System ambayo sheria za Kiislamu zinaweza kutimika. Hizo sheria kama tunavyojua, au wengi wetu tumeweza kusikia, nchini Nigeria nchi ya... ya... Kiafrica hizo sheria zinaendelea kutimika. That is northern Nigeria. Na hiyo sheria za Kiislamu ni Serikali kama yetu ...[inaudible]... ambayo ni Serikali ya Kiafrica sio ya... ya... Wazungu. Ni watu kama sisi tu.

Ni nchi ambayo imeendelea kiwango fulani ya kimaendeleo. Na sio ajabu asubuhi ya leo, hiyo mahakama ya sheria ya Kiislamu inaendelea huko Nigeria. Kwa hivyo kwanini hiyo, hiyo nafasi tusipatiwe sisi kama Waislamu tuweze kuendelea kutumia sheria hizo hapa Garbatula sio pahali pengine. Sio huko Nairobi, Kadhi's Court. Tuweze kutumia hapa Garbatula tukiwa na ...[Arabic]... yetu ambayo wana weza kufanya mahakama. Kama nchi zingine pia za nje. Saudi Arabia, Kuwait, ningeweza kutaja machache Sudan hapa jirani yetu, Iraq na Iran pia wanaendelea kutumia hizo sheria. Na kama tunavyojua hawa ambayo wanatumia hiyo sheria, hawana shida zozote. Ya ulevi, ya wizi, kusema uwongo, hakuna break-ins, hakuna robbery with violence, robbery hakuna. Ukienda Saudi wengi waliweza kutembelea labda Sheikh Ibrahim Lethome, nafikiri ameweza kutembelea. Na huko, nchi hizo au, wale wengine ambayo wali weza kuwa na fursa ya kutembea nje, waliweza kuona nzuri sana sana wale wali enda Hija.

Ni ajabu mtu ana, anazitupa au anaziweka pesa zake huko nje tu, dukani haifungwi, unawacha tu pesa huko, gari yako unawacha huko nje, baada ya dakika tano opposite ya hiyo, kuwacha gari yako Nairobi. Baada ya dakika kumi gari itakuwa imeondoka. Na kila siku, kila siku, watu huko sehemu ambazo za mijini unaona vile matatizo ambazo zinaendelea. Kwa hivyo lakini zile nchi ambazo zina endelea kutumia sheria za Kiislamu hawana matatizo yoyote.

Salama ya kutosha kwa sababu inalindwa na kitabu ya mwenyezi Mungu. Hapana ile paper document, hapana zile ambazo zimeandikwa na binadamu, ambazo huko nyuma zimeandikwa ziko katika kitabu, lakini haitumiki vizuri.

Yangu ya tatu. katika vile tunajua. Katika nchi yetu tukufu ya Kenya wakati ilipo chukuwa atamu ya uongozi, na Bunge zilizo pita, na Bunge za leo pia, ambayo wale wako. Walichukuwa pamoja na hayati Kenyatta na wengine, walichukua ahadi ya kwamba sisi tutalindwa. Lakini mpaka wakati huu hiyo ulinzi hatujapata. Ukienda pahali popote saa hizi, utaona ya kwamba wale ambayo wamechukua ahadi ya kulinda hii nchi, na watu wanaendelea kuuana. Police Station wako pale. Commissioner wa Nairobi... Commissioner wa... wa... Commissioner wa Police ako Nairobi, na karibu na ofisi yake, kila siku maafa ya wizi, na kuuana, na robbery with violence

zinaendelea kuwa huko Nairobi. Kila pahali. Whether it pleases or displeases anybody this is my chance please.

So now, hizo ndizo ambazo zinaendelea kuendelea. Lakini je! kama tungeendelea kutumia hiyo mwizi, ambaye ameiba, na tuendelea kukata amputation of hands, huyu hata weza kurudia kuiba tena ...[inaudible]... Alcoholism uvutaji ya bhangi, corruption, all those social evils will be eradicated or will be minimized. Kama tunaweza kutumia kurudia katika utimiaje wa, kurudia, kutumia maneno ya mwenyezi Mungu. Kwa vile tume abandon ile maneno ya mwenyezi Mungu, ndio mambo zinaweza kuendelea. Hata na omba ati kwanini ni si seme nchi nzima za Kenya itawaliwe na dini ya Kiislamu na Koran tukufu. Ili tupate matumizi, pesa mingi zimetumiwa, alot of money has been used.

Com. Muigai : Propose please, propose please.

Mr. Hussein Roba : Pesa ambazo...

Com. Muigai : Propose. Make a proposal.

Mr. Hussein Roba : Ningeomba kutoa...

Com. Muigai : And summarize.

Mr. Hussein Roba : Nchi hizo, Katiba zinaendelea kuwa marekebisho hii ya nchi ziweze kuendelea kutumia katika sehemu fulani. Sana sana sehemu ambayo sisi Waislamu tuna ina fit zaidi, kwa wingi. Ningependa kama sio nchi mzima tuweze kuendelea kutumia sheria hizo tukiwa na... pamoja na Maulana wetu waweze kuendelea... waweze... waweze... kuendelea hizo, kuendelea hiyo dini.

Com. Muigai : Okay

Mr. Hussein Roba : Mwisho kabisa labda, tafadhali utanisamehe kidogo, mambo ya afya, maji, na mengine mengi ambayo singeweza kutaja, na wengine mimi na jua hakika wao watakuja nyuma yangu au wametangulia kusema wale ma... ma... ma... mapendekozo tafauti tafauti. Kama vile afya. Mtu akiuguwa saa hii ugonjwa. Hapa hospitali ya Garbatula Sub-District mnaona wenyeji wakisikia Garbatula Health Centre, au Sub-District, labda kwa wale ambayo ni wageni. Wanafikiria ni hospitali kubwa ambazo watu wanaendelea kupata huduma mbali mbali. Lakini kwa hakika wenyeji wanasikia, katika mioyo yao au katika masikio yao wakisikia Garbatula Sub-District. Saa hii uki enda hospitali kubwa ambazo watu wana endelea ku pata huduma mbali mbali. Lakini kwa hakika wenyeji wana sikia, katika mioyo zao au katika masikio yao wakisikia Garbatula Sub-District. Saa hii

ukienda, moja labda wageni hawa wetu wakiwa mgonjwa hatuwezi kupatia hata aspirin saa hii hapa. Na the same Government is there, the same service, the same Ministry of Health is there the same Mo which is there...

Com. Muigai : Propose, Propose.

Mr. Hussein Roba : Kuhusu hizo ningependa kupendekeza pesa ambazo zili kuwa zimetumiwa... zikitumiwa huko Nairobi, au huko Embu, sisi tuweze kupatiwa, tujiweze kuendeleza, hiyo pesa allocation tupatiwe sisi wenyewe, bila kulaumiana sisi wenyewe, tupatiwe hizo pesa hapa tuwe na kamati yetu, kama kawaida, iwe ya hospitali irudi katika decentralized. The service should be decentralized, as my suggestion.

Labda sijui kama itakuwa ya mwisho, utanisamehe Bwana, your Honour Commissioners. Ya mwisho ni juu ya employment. Mnajua katika nchi hii yetu kila moja, kila asubuhi, gazetini, kwa radio watu wa... unasikia ya kwamba, kuna ile upungufu, au ukosefu ya kazi. Lakini ukosefu ya kazi, kwa... kwa... in my view, hiyo ukosefu ya kazi, kazi yote imeletwa na corruption. Kenya, kama vile nimeweza kusikia, au tumeweza kusikia kulingana na ile Un, World Rating is one of the second or third corrupt country in the world.

Com. Muigai : Okay, proposal.

Mr. Hussein Roba : Na hiyo taabu yote...

Com. Muigai : Proposal. Proposal please. Proposal.

Mr. Hussein Roba : Hatuwezi... kuweza kupunguza hizo corruption, kuweza kupunguza hizo corruption, kama vile nimeweza kutanguliza. Corruption ile dawa yake ni kutimi... utimiaji au kusimamisha dini ya haki ya mwenyezi Mungu na kurudi... turudie tuweze kupa... kurudishwa katika utumiaji wa Koran tukufu. Hiyo ndio inaweza kumaliza corruption. Kwani corruption, mtu hawezi akaiba, mtu hawezi kuhongana kwa sababu anaogopa mwenyezi Mungu. Lakini bila hiyo hatuwezi kuendelea. Hiyo mambo itaenda, inaweza kuendelea na itaenda hata vizazi zijazo wataendelea kupata shida vile tunaendelea kupata.

Com. Muigai : Okay. Wakati umeisha, tunapatia kila mtu dakika tatu, tatu kwa sababu tuko na watu hamsini-na-wawili wanataka kuzungumza.

Mr. Hussein Roba : Haya asante sana your Honour Commissioners. Thank you very much.

Com. Muigai : Asante. Sheikh Ali. Dakika tatu Mzee, tafadhali.

Sheikh Dabaso Ali Dogo : ...[Arabic]...

Com. Muigai : ...[Arabic]...

Sheikh Dabaso Ali Dogo : Mimi nina mapendekezo machache sana.

Com. Muigai : Asante

Sheikh Dabaso Ali Dogo : Kwa majina naitwa Dabaso Ali Dogo.

Com. Muigai : Sheikh Dabaso

Sheikh Dabaso Ali Dogo : ...[eEh!]... Kwanza kabisa, mimi nimefika wakati ya ukoloni, nimezaliwa, nilikuwa mkubwa. Na wakati huo, Serikali ilikuwa mbali sana na sisi, na hata elimu hatuku pata. Lakini wakati Serikali ilikuja, tulipata Serikali yetu yenyewe, ndio shida ilianza, kwa sababu sisi tuka sema, sisi hatutaki kuwa katika Kenya. Sasa sisi kama raia tu ya Serikali hii badala Serikali kutafutia sisi solution ya kushika sisi mzuri. Serikali ili tumaliza kabisa pamoja na mali yetu, na sisi tukawa maskini, mpaka wa leo. Kitu ya kwanza, nataka Serikali itulipe ridhaa ya hiyo mali wetu, na watu yetu ambao walimalizwa wakati ya Emergency. Hiyo ni moja.

La pili, sheria ya sasa inasema ardhi hii, ni yako juu, ndani ni ya Serikali. Hiyo sheria... sheria hiyo iondolewe kabisa ardhi iwe ya wananchi. Kila kitu ile inapatikana juu na ndani iwe ya community hiyo. Kwa mfano kama vile leo iko... iko... iko dhahabu hapa Duse iko mawe, precious stone hapa. Hiyo mawe sio yetu. Sasa leo tumekosa say, hatusemi, hatuna uwezo. Kuna watu wamechukua licence yao wanakuja kuchimba, na ni yetu, pahali... mimi mwenyewe nimezaliwa pale.

Mimi kama Councillor leo, hatuna uwezo ya kuandika mtu moja katika Council, mpaka Minister aweke signature yake. Kwa hivyo County Council ipatiwe nguvu.

Mali tuko nayo ya kutosha, na ardhi yetu iko na rutuba ya kutosha, tunaweza kulima, tunaweza chunga mali yetu kila mahali. Lakini mipaka yenyewe hatuna. Mipaka ya ukoloni, wakati ya ukoloni, kutoka Isiolo ilikuwa maili nane, leo iko katikati ya town. Tunataka hiyo mipaka irudishwe pahali yake. Kila mahali kama wakati ya ukoloni.

Nikikumbuka vizuri, wakati wa ukoloni, watu wawili wali uwawa huko Merti vijana waliuwawa watu wawili, wakatupwa ndani ya maji. Maiti ilienda mpaka Abaswe Maiti ilishikwa huko. Wakati huo wa ukoloni wazungu

walisema, wauwaji waletwe, na wakaletwa. Leo hii, mimi natoka Markadaka watu sitini-na-tano wali uwawa bila Serikali kufuata hata nyayo moja. Kwa hivyo nataka mipaka irudi pahali yake watu waishi katika sehemu yao bila kuogopa.

Kwanza kabisa, Serikali ije karibu na sisi. Leo vijana hawa wote hawana Id card, hawana Identity Card, na mimi nataka kura kwao. Nita pata namna gani. Hawana Identity...Identity. Kwa hivyo, kwanini Id hapana wekwa katika ofisi ya Chief yote, location yote, iwe na Id, iwe na Passport, hapo hapo tu pate. Hiyo ni kuonyesha Serikali iko na sisi. Leo hii hatuna Serikali.

Serikali hapana iko, nauna ogopa hutasema. Watu wakimalizwa, wewe kama Councillor, ukisimama hapa, unambiwa usionge habari ya security. Na ni watu wali kwisha jana usiku. Security hiyo kama Serikali hapana weza kulinda sisi, sisi tununuwe bunduki yetu, ihalalishwe. Tujichunge.

Viongozi tunataka hata ma Chief tuchaguliwe, tuchaguwe wenyewe. Sisi tuchaguwe Chief ile tunataka. Sio kuwa imposed. Kuwekwa juu yetu. Mtu fulani ambaye, kama mimi nikitoka Markadaka ninaweka ile kijana na fanyia mimi campaign sana, awe Chief ya huko. Hapana hivyo. Wacha wananchi wachaguwe, wafanye kama ni mlolongo, kama ni kura ya siri, ma-Chief wachaguliwe na watu kama vile Councillors wachaguliwa, kama vile mjumbe anachaguliwa. Na tuwe na uhuru wa kuchaguwa.

Katika kulipa hiyo ridhaa, ambayo niliyopitia hapo mbeleni. Tukisema leo tulipwe ridhaa, leo miaka hii, tuko, 2002 inaitwa dotcom. Dot maana yake ni pahali maneno ina malizikia.

Com. Muigai : ...[ha! Ha!]...

Sheikh Dabaso Ali Dogo : Sasa hii dot, yote wataandika... waka se... kila mtu atasema Baba yake aliuwawa, ng 'ombe yake ilichukuliwa. Kwa hivyo kupoteza hiyo yote, wacha Serikali itupatie elimu ya bure miaka ishirini. Sisi kama Waislamu, hata leo ingawa tu, ni sheria inakubali tunasimama hapa. Sisi tuko na Constitution yetu ambaye imekuwa written. Ime... ime andikwa na mwenyezi Mungu, ime... ime... ime ongewa na mwenyezi Mungu ambaye inaitwa Koran. Hiyo ina hukumu kila kitu. Hakuna hukumu hapana haiko ndani yake. Hukumu yote iko. Tu ki... sisi Waislamu turudishwe katika ku... hukumu hiyo, tufuate Koran. Koran ituhukumu kwa kila mahali. Makadhi wawekwe kila Location, na wapatiwe nguvu ya kutosha wa hukumu sheria ya Kiislamu.

Leo hii tuki taka kuongea, mambo mengi watu wanaambiwa musiogope kusema. Kwa sababu kama vile mimi na juu. Kama mimi sasa ni Councillor, ni Councillor wa Kanu, nikijaribu chama kingine wananchi wataambiwa we, mutamalizika. Hata kama Kanu ni mbaya, nitakuwa pale tu. Wananchi wamalizike, wafanye nini, ni hapo hapo tu,

kwa sababu, nikiondoka sitapata kura. Kwa hivyo, wananchi wapate uhuru wa kutosha katika ardhi yao, wafanye vile wanataka, bali tu wasivunje sheria.

Kwa hivyo sisi tunataka, hasa katika sehemu ya Waislamu. Tupatiwe shi... tupatiwe tujhukumu katika dini ya Kiislamu. Leo kuna Kadhi katika Kenya, wengi sana, lakini hukumu yao ni urithi na talaka peke yake. Hawafanyi kazi ingine. Watu wana weza kufa hapa, mtu ane... anaweza kuiba, na pia isitoshe, kama huja ridhika, na ardhi katika District yako. Lazima uende kwa kufanya Appeal kwa Judge ambaye sio Muislamu. Atakwenda kuhukumu nini sasa? Ana hukumu vile anataka. Na vile anataka, kama leo hii, katika Kenya, vile anataka ni vile pesa uko naye. Kiasi ya pesa ile uko naye ndio atahukumu. Kama sisi tutaenda wapi. Mali hatuna, hatuna uwezo, watu wengi, kama vile Mzee alikuwa mbeleni yangu hapa anasema, hawana Id card, hawa... hawezi kufika Isiolo, kwa sababu ya transport. Serikali hapana iko hapa. Ata fanya namna gani? Kwa hayo machache na shukuru sana, na ningependa mapendekezo yangu hiyo ichukuliwe vizuri. Asanteni sana.

Com. Muigai : Asante Mzee. Bonaya Racha. Bonaya Racha. Dakika tatu Mzee. Tafadhali.

Mzee Bonaya Racha : *Saallammaalleykum, annii nii dhuubbin tiyyaa dhiiqoyyo, maaqaan kiyya Boonayaa Raacaa, gaafaarssa duufee*

Translator : Mzee anasema anaitwa Bonaya Racha, anatoka sehemu za Gafarsa.

Mzee Bonaya Racha : *Aannin beendekeezoon tiyya, akh maalee diiqaayoo*

Translator : Mapendekezo yake ni machache.

Mzee Bonaya Racha : *Nuu gaaf duurri kaanii, gaafaa koolooni, naamii cuuftii fuulaa uuffi qaabb.*

Translator : Zamani anasema kila moja alikuwa ana sehemu yake wakati wa ukoloni.

Mzee Bonaya Racha : *Booranii guuyyaa suun, akh maalee maaniikan, naam aakkhammalee uhuuruu qaabb*

Translator : Wakati huyo tulikuwa na uhuru ya kutosha katika hiyo nchi yetu, na mipaka yetu.

Mzee Bonaya Racha : *Aammalee nuu guuyya suunii akhii nuu uhuuruu qaamnuu, naamii cuuftinuyyu laaf uuffi qaabb*

Translator : Anasema kila moja alikuwa na sehemu yake.

Mzee Bonaya Racha : *Guuyya naamii laaf uuffii qaabbuu naagga guudhoo qaabb*

Translator : Mtu akiwa katika sehemu yake ana amani ya kutosha.

Mzee Bonaya Racha : *Hoorrii issaa gaauu qaabb*

Translator : Atakuwa na mali ya kutosha.

Mzee Bonaya Racha : *Guuyya suunii diibbi nuu irraa qaamuu illiimuu caalaa nuu dhiiqoo*

Translator : Zamani ili kuwa ni elimu tu inatusumbuwa.

Com. Lethome : Mapendekezo.

Mzee Bonaya Racha : *Ammaa woonii ann feeduu, haagg nuu siirkaal keenyaa khaan dhuunee, nuu diibb guudhoo irraa aarggan, diibbi nuu aarggaanee, hoorri kheen suuniif laaf teen suun cuufaa siirkaala nuu daaggaanyyi, ammaa akhii ann feeduu, khaa laaf teen suulle, haagg seehemmu teenaa khaa akh laaf siyyoloofaa, siyyoloon laaf booraanaa jeedaani maaqaa booraanaatin issin teetuu. Khaa khaan lee naam dhuurri hoobbaeef hoorri dhuurri nuura hoobbassani cuufaa ammaa taan maanikhan siirkaalii khaa nuu dheebbisuu jeed*

Translator : Mzee anapendekeza anasema, ya kwanza Serikali ifanye bidii katika Katiba tuhakikishie mipaka yetu ambayo imenyakuliwa irudi. Ya pili anapendekeza ya kwamba Isiolo District iitwe Borana District. Ya tatu Mzee anapendekeza ya kwamba mali yetu pamoja na nafsi, ambaye iliuwawa wakati ya Shifta War, tulipiwe ridhaa.

Mzee Bonaya Racha : *Nuu aammalee loon qaamnaa khaa nuu loon qaamnuu, loon kheen suun uufumaa qaamn maalee haaqqi tookoolee irraa inqaamn. Aakhii ann feeduu, khaa loon laaf taanaa aammum taan yoo issaan yaan, naamii aamuum taan meeroo taana loon daaqqaat, permit maale indheem, khaa permit suunnileen nuu imbbaaamn, hoorri kheen meenyewee irraa qaamnuu, gaarri guubbaa keeyyacuu indhaandheen, khaa hoojja nuu gaarri guubba keeyyanuu poolis suun manyaaweelee maani khaan hoorri kheen khaan beedheel sookoo nuu aammo hoorrii kheen khaan nuu ammaale gaadheebiinee hoorri khaankhee khaan akhaa waan attiin right ittii inqaamnee, hoorri khaankhee khaan meenyewee siiraa nyaataan. Khaa aammaantaana sookoonii Sub-District kaanaa nuu dheebbituu*

Translator : Mzee anapendekeza ya kwamba Katiba yetu, leo sisi watu wa mifugo tukitaka kupeleka mali mpaka Nairobi, mpaka mtu akate permit, sijui nini, no objection tupeleke, hata hiyo. Pamoja na permit yako hupati usalama. Utakuliwa njiani, mpaka hata utoke ngozi na nyama yote.

Com. Muigai : ...[ha! Ha!]...

Translator : Anasema tunataka soko iletwe hapa katika Sub-District ya Garbatula, soko ya mifugo, vile zamani ili kuweko.

Mzee Bonaya Racha : *Gaarbb-tuulaan khuuniini, gaaff dhuurri khaanii khaa maaqqan issaa location haaqqii guudhoo qaabb, waan siirkaalii qaabb cuufayyu inni inqqaabb, ammoo sub-district jeedaanii maaqqaa caalaa qaabb, distrptic jeenaanii woonii qaarra khee jiirra cuuftillen kheessa goodhaant, khaa ammantaana, yoo innii sub-district taat, waan qaarra khaa kibbandheen aarm nuu duuftuutii*

Translator : Mzee anapendekeza anasema ya kwamba, zamani wakati Garbatula ilikuwa Location, ilikuwa na kila kitu. Ilipofanywa kiwango ya Sub-District, hata ile kitu yote sijui imeenda wapi. Maendeleo yote ikabomoka. Kitu ya kwanza ana omnia kipande iwe hapa katika Garbatula Sub-District.

Mzee Bonaya Racha : *Nuu naamii ammantaanaa naam ggaan soodhoomaat khaa kibaadhee inqqaamb jiirr, khaa kibaadheen tuunaayyu kuurran iillingaan, khaa issin kuurraan illingiinee khaa oofiis issi aarm qaabdhee guuyyaa cuufaayyu maanii khaan, taa kibaadhee teen diiraamaa gaalgal cuuf, kuurraa woolt illiingiinee kibaandhee teena akh haaqqiin keenyaa diibbin qaabdhuu nuulen khaa qaamnuu oofis*

Translator : Mzee anapendekeza, anasema leo kipande mtu akitaka, mpaka ina ngojewa wakati ya card ya kura itakatwa, ndio sisi tunapewa kipande, kama wananchi ya Kenya. Hatutaki hiyo tunapendekeza, katika... Katiba yetu itupatiye nafasi kila siku ofisi iwe hapa mtu akitaka kipande anaweza kukata wakati yoyote.

Mzee Bonaya Racha : *Kwaa saababuu Chief aarm innjiirra, Muujumbeen injiirraa Councillor aarm injiirra maaqqummat aarm jiirr maale, woonni tookoolen khaa Council waalaa Chief haarkaa qaabb injiirtuuUtaawaalaan teen guubbaa caalaa jiirtii khaa guubba injiirree, siirkaalaaf nuu woolt gaadh duumnee woonii kheen cuuf khaa woolt maalaanut*

Com. Muigai : Summary. Summary.

Translator : Mzee anapendekeza anasema ya kwamba leo Serikali ime kuwa mbali na sisi. Tunataka Serikali ije karibu na sisi, hapa hapa pahali tulipo.

Mzee Bonaya Racha : *Wonnii issiin akhaasitiifii, nuu aammuumtaan woonii nuu haaqqii daamn jeenuufii, nuuf siirkaal gaargaar jiirr, maaquumaa nuu biirr jiirr maalee siirkaalaaf nuu woolt indiyyan, saababuu adhaa dhuurri khaani adhaa misingaafaa, adhaa buunaafaa adhaan woorr loonii taakaayyu intaan, nuutii dhuurri haaqqi irraa qaabbn maalee haagg aamoo nuu adhaan teen woolt dhuudhee, hoorri kheen suun adhaa inqqaabbuu, woonii hoorri kheen maanyaaweele nuu waan tookoolee deefee irraa daamneef haagg suun*

Translator : Anasema leo kuna Act, kuna labda sheria, na katika Katiba, inajulikana mimea fulani, kama ni kahawa, kama ni majani chai, nini... Katiba inachunga. Kuna Act yake. Tunataka Act ya mifugo iwekwe ambaye inachunga masilahi mifugo yetu, na soko yake na kila kitu, iingizwe katika Act.

Mzee Bonaya Racha : *Aamm waan ann feeduu, siirkaalii gaaffaa beetta nuu hoobbaan sunii, aahaadhii saadhii fuudee, aahaadhiin saadheen innii fuudee illimu burree issaanii kheenaanjeedaan, raayya aammalee beelaan indhoot jeeedaan, hoorrii raayya aammalee hiinttiisaan jeedaan, woonii suun tookoolen intaane, kha ammaa taan kaatibaa khee nuu khaanii illimu teenalee baakaa gaan dhiidhaama illmaan buurre nuu soomsisaani, hoorri kheen khaa hoobbassanilee [inaudible] nuu kheenaanii, hoorri kheen ammalee akh dhansaa nuu tiissan, tikhii hoorrii kheenaa woonii nuu inqqaamnef, maal miisinqaa haarkaa qaabbuu nuunii maalaacuu jirraa, suuniinitii ammaalii kheen woolin taaee wooni cuuf khaa haark kheenaa dheebbitu*

Translator : Anapendekeza, anasema Serikali wakati tulipata independence tuliahidiwa mambo matatu. Tuliambiwa tutapewa elimu ya bure, tukambiwa tuta... mtu hata kufaa na njaa. Tukaambiwa mali yenu na nafsi yenu itachungwa. Hizi vitu tatu yote haikutimizwa. Kwa hivyo Katiba hii mpya ihakikishe ya kwamba tuna pewa elimu ya bure, na anapendekeza mpaka mwaka ishirini, kwa vile sisi mali yetu, na kila kitu yetu ili malizwa wakati ya shida. Tulipwe elimu ya bure, tufundishwe kwa miaka ishirini. Na ihakikishe Serikali imetufanyia food security ya kutosha na pia anasema mali yetu na nafsi yetu iwe protected ya kutosha. Na sisi mifugo yetu itambuliwe kama vile mimea ingine inatambuliwa.

Mzee Bonaya Racha : *Aammaa wonii anniin, jeech took caalaa naa haafee tookootii taan njeedaa, woonni annin jeeduu, kaaraa khaan nuu guuyya cuuf soobbaan nuu fiitaan, guuyya raayyissi duuf cuuf nuu waan jeedan laaftii siyyoloo tuuniini kaaraa issii laamii daan jeedan, nuu aammoo beedhel laamii kaaraa kheen haalkaaniif guuyya cuufaa, guuyya bookeeni roobbuu, naamii dheebbiye fuullu inggaal, ijjoolen*

skuulla, ijooleen laaf taanaa maa jiidh jeedaanii, guuyya roobba cuuuf issin woorr kheesaa ceeleewit kaaraan injirruu, dheerejaani injirru, nuu aarmmaatifii woorri Gaarbaatif woorri Maartii muusiyyanoo tookoolee woolt inqqaabb, maan jeenaan, kaaraat injirreeffi akhaassii, laaziimaa kaaraa suun khaa yoo akhaalee dhaadaabban akh khaara Marsabit tiifaa maarraamu itti faacaassanii suun toolcaanii dheerejaan khaa nuu daanii

Translator : Mzee anapendekeza, anasema leo, sisi katika Isiolo sehemu yetu hii ya Isiolo South, na sehemu ya Isiolo North hatuna mawasiliano. Kwa sababu daraja ili kuwa inaunganisha kati yetu hapa, imevunjika. Miaka na miaka inaenda tuna ahidiwa, na hakuna kitu inatengenezwa. Tumeahidiwa barabara hii mara mingi, hakuna kitu ina tengenezwa. Tumeahidiwa barabara hii mara mingi, hakuna kitu inatengenezwa. Watoto hata wakati ya kuenda shule wanapata shida. Anapendekeza tutengenezewe barabara, zetu na madaraja ambazo inatuunganisha kati yetu iweze ii... itengenezwe.

Com. Muigai : Okay. Saresa Farole Mar. Hebu weka dakika tatu tatu, tatu tatu. Tuko na watu: Eebu weka dakika tatu tatu.

Translator : *Waan issan taataan caaqqassa raalithi qaabbadaa*

Com. Muigai : We have seventy people.

Translator : *Waan nuu taan nuu naam kaarribuu toorbbatamma aam naamii maaqqa qooraat qaarraa, khaa diibbileen gaadh yaauu jiirr*

Com. Muigai : And don't repeat what has been said please. Don't repeat what has been said...

Translator : *Dhuubbi qaarra naam jeejed guudhoo itti indheebbiyyina, diibb dhuurrilee nuura laakiissa, maoonum taante baas, naamuu daaqiqa sadhii qaabb, dhaaqiigan saadheen taante hoobbat aarmaa sii baassanii, daatee uuffirra teeta*

Mr. Saresa Farole Mamo : *Asalaam Aleykum,*

Com. Muigai : Ndio kila mtu azungumuze.

Mr. Saresa Farole Mamo : Mimi... mimi kwa majina naitwa Saresa Farole Mamo I represent youth kutoka Gabarsa. Mimi ni kutoka Gabarsa. Ni mzaliwa wa Gabarsa Sasa mimi niko na maoni mawili. Ambayo... ambayo

inaweza... inaweza ku... kuwa mrefu kidogo.

Com. Muigai : ... usi...

Mr. Saresa Farole Mamo : Maoni ya kwanza...

Com. Muigai : Three minutes.

Mr. Saresa Farole Mamo : Maoni ya kwanza inahusu mambo ya... mambo ya sisi hapa. Watu wa Pastrolists ambayo tunaishi hapa. Nikisema "Asalaam Aleykum", nina shituka zaidi kwa sababu naona ya kwamba ninasema Asalaam Aleykum, kwa nchi ambayo haikubali mimi niseme Asalaam Aleykum. Kwa hivyo mimi nataka hii Katiba ituwekee... ituwe... itu-represent ya kwamba mambo yetu, tabia yetu, dini yetu iwe inaonekana ya kwamba tuko na watu ya Waislamu na tuko na watu ambayo wanaitwa Waborana, Cushites ambayo wanaishi area hii. Kwa hivyo mimi naomba sheria ya cultural behaviour yetu isiwe cultural behaviour ya Bantus, kwa hivyo culture yetu irrespective. For instances our laws, we have got our laws. Tuko na sheria yetu kama Waborana. Constitution must cater for us as a community, sheria ya wa Borana.

Ya pili, na... ya pili nataka compensation kutoka Serikali ya... ya... ya... wakoloni ya... ya watu nyeusi. Zamani tulikuwa na mkoloni mweupe, mzungu, baada ya... baada ya mzungu kuenda. Watu wengine ambayo wanatoka Central Province, na watu kutoka Nyanza. Walichukuwa uhuru. Hiyo uhuru hawaku tuchukulia. Walichukuwa ili wa tu nyanganye. Sisi wengine tume fanyua refugees in our own Country. Leo hii nikienda Nairobi mtu kutoka Nyanza hawezি kuulizwa kipande. Lakini mimi ni Mwaria, kwa sababu ya ujinsia ya nywele, nitaulizwa kipande. Kwa hivyo hizo mambo zote mimi nataka sheria isimamishwe na watu wasituulize kipande. Kurahisisha hiyo mambo za kipande, mambo za Passport, mambo za kitu ya kupigia kura nayo. Hiyo yote ipunguzwe sisi tu patiwe Passport ambaye itafanya hiyo kazi yote pamoja, ya kupiga nayo kura ya kupiga nayo kura, ya ku... for identification and for travelling purposes all those things, those three documents to be removed and then us to be given a Passport for free... for free movement.

The second issue... the second issue, I was reading in history that after uhuru some people from Central and Nyanza were given Canadian Airlift and Russian education. They were taken for education to America, the Tom Mboya issue... Tom Mboya and Odinga but for us we were left deprived of our livestocks'. Now, we need a special attention better than other Kenyans. Afford... a very serious one. We need to be given special attention the way they got their Canadian Airlift and the Od... Odinga Russian education... Pole niko na...

The third issue... the third issue is, mimi nataka autonomy autonomy from the other parts of the country, because

we are now becoming vulnerable to the emerging of the other bigger population like the... the... the Central for the Gema people, the Luo and the Nilotes in the other parts of the country. Sisi hapa tukienda na... na democracy ile ya watu wengi kupata vitu nyingi, hata tukienda Bunge hatuna maoni yetu huko. Kwa hivyo ile maoni yetu ipatikane. Zonal decision making, area watengeneze decision yao. Lakini other parts, because we have to share some parts, like the roads in Central Province and the Universities and the Kenyatta National Hospital and other parts, we all built it together, we should share that together but in decision making we need autonomy from the other parts. These one will create trust between us as a Nation and... and... and bring cohesiveness between us and those from Central Province and Nyanza whom I always take to be my enemy.

Second one I am sorry to say please. Kama ni mewaudhi... the a... a.... another issue, Mr. Githu pole. Another issue like Kbc, this is a nation divided amongst itself. You go to Nairobi today you will find a Nation Tv, Ktn. Then you go to ...[... ? ...]... you hear those and everything. Sasa tukikuja hapa, hapa upande hii yetu ni Kbc, and the Kbc, its advertisement is beer.

Com. Muigai : ...[...ha Ha! ha...].

Mr. Saresa Farole Mamo : Which is a cultural pollution. We should be given what is due to us, and what is not due to us, not to be given to us. Like those beer advertisements, ...[... ? ...]... in that place. It is a cultural taboo to us. Lend us what we want like Ikra Fm and kiboko ya Kiborana matangazo ya Kbc iwekwe.

Ya tatu... ya tatu tafadhalini sana, kama sisi tunataka kuwa cohesive Kenya, hii Katiba... the other time hatukuwa tunasikizwa... tume mo... we have been molested and we were... we were scared and that's why we were keeping quiet. Now you have made us talk. We shall talk and react. If you don't us wan... if you don't want us to react... the way Coffee Board, Tea Board, Maize Board all these are there. There must be Meat Board for Camel. That what people don't want to hear. Meat Board, Pig Board and Sheep Board all those things must be there. And it should... it should not be some people deciding for us in Nairobi. There is no representation without taxa... there is no taxation without representation. You are taxing us and you are not representing us. It is Mwangi, Lu... Otieno, Owino taxing us, without represent... without knowing me. Somebody has never gone to Gabarsa and he is talking of Gabarsa. That's bullshit or cumbersome?

Com. Muigai : ...[...ha Ha! ha...].

Mr. Saresa Farole Mamo : Another issue again, at hand. Another issue which I want to say is this. There is forced labour in this part of the country. Forced labour is there. We employed some people to defend us from foreign enemies. There're some people whom we employed to defend us for internal security. These people

have abdicated there duty, the Police and the Ap's, the few we have are being collected to the... these days especially to the Rift Valley. The Police and Ap's. We are given Home Guards, I think in my English Home Guards means guarding your own home. Now the Home Guards, the Police are just sitting here when livestock are being stolen from other parts, somebody comes... who is not paid... he is told now, why didn't you go and catch those... those thieves. They have been given shoddy... shoddy arms, and the other ones have got automatic rifles. These guys go and die, the insurance is... don't cover them, they are not paid for that, they don't work for ... for that, then labour without any profit.

Such issues especially, if the Police can't be able to attend to our issue, let their be Community Police, paid by the Po... paid by the Central Government. Especially the Police and the Administration Police. The Colonialists I heard from my Grandmother, the Colonialists used to employ our own Administration Police, and they used to guard our internal security. Now it is the foreign Police who are... who is born... who has no mistake... who was born in Central Province, who doesn't know these climate. Who is told to work in this desert, that's very hard for him to... To ease all that I propose an Administration Police Line which is under the Government arm, which is Community based ...[inaudible]...

Com. Muigai : Summarize please, summarize please.

Mr. Saresa Farole Mamo : Devolution of power I think I have talked about that. We need to be taken from that part of the country. Our cultural law should be catered for. Those are the things I been... I have in mind.

Com. Muigai : Thank you.

Mr. Saresa Farole Mamo : And the... please don't forget to give us the Canadian Airlift, this one we must be given as special attention. Or else a special mutiny of special educated people or a revolt, I am sorry to say might arise. Asalaam Aleykum

Com. Muigai ...[...uHu!...]. Abdi Galgalo.

Translator : Next, nani Abdi. Abdi Galgalo.

Com. Muigai : ...[inaudible]...

Mr. Abdi Galgalo : Asalaam Aleykum, mimi na maneno... Mimi ninaitwa Abdi Galgalo kutoka Kinna. Nina maoni mbili, kidogo, fu... fu... fupi. Kwa hivyo mimi ni tofauti na huyu sasa vile amesema. Mimi niko tofauti

kidogo vile alisema, lakini natoa maoni yangu. Maoni yangu, sisi tumesikia wakati Kenya ilipata uhuru miaka thelathini-na-tisa, tumesikia uhuru tu kwa mbali, lakini hatujawai kuona, watu wa sehemu hizi. Kwa hivyo wakati tumepata uhuru ndio sisi tumepata ukoloni. Shida tumeanza wakati huo mpaka sasa. Watu wengi wetu wameuliwa na Serikali, wameuwawa na Serikali, watu wetu wengi wameuwawa na Serikali, watu wetu wengi wameuwawa na Serikali mpaka saa hii mazee kwa hivyo... kwa hivyo wacha ...[inaudible]... kwa hivyo wakati hii Katiba mpya hii tupate uhuru.

Wakati wa mbele hatujapata. Wale walipata uhuru ndio hao sasa... hospitali, barabara imetengenezwa, kila mahali, shule, maji, ndio wamepata. Sisi sio wengine... Kenya Serikali, vile sisi tumezaliwa nchi hii, wacha tukae, wacha wakae tu. Lakini hawana haja na sisi. Hakuna haja kidogo hata na sisi. Kwa sababu wanyama wa pori ndio wako haki kuliko sisi. Wanyama w pori iko haki kuliko sisi. Kwa hivyo mimi nataka Katiba mpya yetu, upate haki yetu, tupate haki ya kibinadamu. Kwa hivyo watu wengi wamefariki najua kwa muko wa Serikali, hapa sisi tuna... hatutawuliwi na sheria... hakuna sheria, tuna tawaliwa na bunduki. Mtu anauliza kitambulisho anaweka bunduki kwa mdomo. Unasikia. Mimi nikiharibu kitu, halafu nienda pahali fulani, ni toroke, mna kuja kwangu nyumbani. Wakikuja nyumbani, kama watoto, mama, wasichana, wazee... wale wako nyumbani, mtu anaye husu hiyo... shi... mme fanya. Yule mtu ametoroka, lakini wale walioko nyumbani, hawapati usalama. Hawa ndio wanateswa, nawekwa ndani, na nyanganywa, naporwa mali yao. Na hii Serikali ndio wanafanya hivyo. Hapa bunduki ndio inatumika sio sheria inatumika. Kwa hivyo tupate haki kama wakenya wengine. Kenya... sheria Kenya inasema, mtu akifanya makosa, muguse yeye ndio ana tafutiliwa, hata kama ni miaka kumi, yeye ndio anatafutwa. Lakini sasa hapa hakuna. Mtu mwenye makosa akitoroka, hiyo kabilia ndio... mlango yake ndio imepatwa. Hiyo sasa... hiyo tafadhali iongezwe katika Katiba mpya. ‘Asalaam Aleykum, Warahmatulah Wabarakatu’.

Com. Muigai : Asante sana. Mohammed Guyo. Mohammed Guyo dakika tatu tafadhali. Na usirudie sana yale tumesikia, tumeandika chini.

Mr. Mohammed Guyo : Asalaam Aleykum, mimi kwa jina naitwa Mohammed Guyo. Nita toa mapendekezo, moja, mbili, tatu hivi. Ya kwanza...

Com. Muigai : You know we have only done...

Mr. Mohammed Guyo : Nitatoa mapendekezo kuhusu mifugo. Sisi hapa, uchumi wetu unategemea mifugo, hatuna mashamba makubwa, hatuna mashamba ya kahawa, ya majani, ya kupeleka factory. Lakini ile kitu tuko nayo ni mifugo. Na hii mifugo yetu kuuza inakuwa shida sana, kwa hivyo kila mara kuna kitu kina itwa permit, la... mpaka tupate hiyo permit, haya... sheria haiwezi kuturuhusu kupeleka mifugo yetu mahali tunataka. Na hiyo permit, hii area yetu inaitwa Cdpp area, iko kitu inaitwa quarantine, kila miaka Cdpp hiyo area, hatupatiwi hiyo

mpaka ng'ombe inachukuliwa damu. Hatupati hiyo permit. Kwa hivyo tunataka hii sheria ambayo itakayokuja vile nimependekeza. Kitu inaitwa quarantine ipigwe marufuku. Mifugo kama iko ugonjwa itibiwe na sisi tunapata permit wakati inayotakikana yote karibu na sisi.

Ya pili, sheria ikubalie sisi nimependekeza tupatiwe soko ya mifugo yetu tuweze kuuza nchi za nje. Tuweze kuuza vile bidhaa hizi zingine zinauzwa, tuwe tukiiza nje.

Ya tatu, nitagusia juu kidogo ya mambo ya ardhi. Hii ardhi yetu inaitwa Trust Land. Hii Trust Land, hii jina iondolewe iitwe Community Land. Jukumu iwe yetu, sisi tuwe na jukumu ya hiyo ardhi, sio ati watu wanaenda ofisi huko juu, Commissioner of Land anapeana barua kwa mtu yule yoyote ambaye hajawai kuona pande hii. Ame patiwa barua na Commissioner of Lands ati anakuja, anataka anasema, anataka sehemu fulani ati ni yake. Hiyo sisi imetuumiza, miaka nyingi. Tunataka hiyo ardhi iwe chini yetu, tukiwa pamoja na County Council na tuwe na kamati ya Trust... Board of Trust, kama watu kumi kutoka kila Location.

Ya tatu, nitagusia juu ya uchumi. Sisi Waislamu kuna kitu inaitwa, mkopo, ambaye ni ribaa kwa Waislamu kupata hiyo mkopo. Na nchi hii Bank yoyote, ama mahali yoyote ya kupeana pesa, lazima inakuwa na ribaa Kwa hivyo sheria nimependekeza sheria ibuni ya kuleta Bank ambaye haitatoza sisi ushuru... ribaa tusipate interest yaani hiyo ni haramu kwa dini yetu na tusile, kama Waislamu haramu.

Inging pia nitagusia juu ya mambo ya chama. Vyama, tuko na chama nyingi Kenya, mimi kwa mapendekezo yangu tuwe na chama mbili ama tatu katika nchi hii. Hii chama nyingi kama makabila inatu... haina maana kwetu. Chama moja ikitu haribia kitu ingine inatetea. Kwa hivyo mbili, tatu kwa maoni yangu ni mzuri.

Com. Muigai : Yes Bwana Guyo.

Mr. Mohammed Guyo : Yes, ya mwisho, nikiongezea, nitarudia ile mambo ya mifugo. Nataka hii mifugo badala sisi tunapeleka mbali, sasa kuna sehemu ambayo imejengwa ya mahali ya kuchinjia mifugo, upande wa Masaaini huko. Tunataka kitu kama Kmc iwe ikijengwa katika area hii yetu. Tu... tu... tuwe tu... tukiweza kuuza mifugo yetu kwa hiyo Kmc ambaye ni karibu na sisi. Kwa hivyo kwa maoni yangu mimi napendekeza haya.

Com. Muigai : Asante sana. Mohammed Abdulkadir. Mohammed Abdulkadir. Hayuko tu ...[inaudible]... yukoo. Okay karibu, Bwana Mohammed.

Mr. Mohammed Abdulkadir : Hamjambo wote.

Com. Muigai : Karibia mic.

Mr. Mohammed Abdulkadir : Hamjambo watu wote.

Com. Muigai : Hatujambo.

Mr. Mohammed Abdulkadir : Sisi tunataka kuomba kitu kimoja, Bwana Commissioners mmekuja hapa, kwa sababu ya jukumu fulani, na leo ni siku muhimu kwa watu wetu sababu hatuja husishwa kuandika Katiba katika maisha yetu. Tungependa kuomba nyinyi msituharakishe, mtupe sisi nafasi yetu leo sababu kuna watu wengine wanaweza kulia hapa usikie mbaya. Sababu hapa ni hardship area tunaweza kuuliza Serikali ina mpa nyinyi hardship kidogo...

Com. Muigai : ...[...uHu!...].

Mr. Mohammed Abdulkadir : Kwa hivyo, tafadhali tuwe rafiki hapa. Mimi ningependa kuzungumza juu ya Executive...

Com. Muigai : Karibia mic.

Mr. Mohammed Abdulkadir : Juu ya Executive, mambo ya Serikali. Ningependa mtu yoyote anataka kupigania urais wa nchi asiwe mjumbe. Napendekeza hiyo kwanza.

Ya pili, Rais asiwe na kazi ingine isipokuwa ya Executive. Mambo ya Judiciary, mambo ya Legislature isiwe yake. Akae mbali, sababu kitu ya kwanza mtu akiwa yule mjumbe ya hapa south, na niwe Rais, inajenga wapi. Hapa. Mapendekezo ya kwanza, ningependa hiyo, kwa sababu ya kuwa... na asiwe na bias.

Ya pili, mtu yoyote anakuwa President. Qualification ya kuwa President. Lazima mtu ambaye amesoma, amehitimu kiasi ya kufika hata University. Awe President... Presidential candidate must be a graduate. Napitia tu kidogo kidogo.

Com. Muigai : ...[eEh!].

Mr. Mohammed Abdulkadir : Judiciary. Mambo ya Judiciary ningesema. Napendekeza sisi tuwe na Yes.

Com. Muigai : ...[eEh!].

Mr. Mohammed Abdulkadir : The present structure of the Judiciary contains... consists of a Subordinate Court including the Magistrate Court, Kadhis' Court, High Court, Court of Appeal peke yake. We therefore propose the following should be specified in the Constitution. The present structure must be such... the present ... the Judiciary must be structured as below. We need Supreme Court, Procedural Court, Independent Judicial Court. Judicial Officer must be ...[inaudible]... nuu aaffaan boorati yoo attin kizzungu dhuubbat. Haya wale wanafanya kazi ya... kazi ya kotini, ama ma wakili. Lazima wawe wale wame soma na wamehitimu, na wamesoma mpaka University. Sababu kuna wakili... I mean... kuna majudge wengine wanatolewa huko huko, wanakaa ndani ya Kotini na kazi ile wanafanya hairidhisi wananchi...

Com. Muigai : ...[...uHu!...].

Mr. Mohammed Abdulkadir : Kwa hivyo Ju... wale wanafanya kazi ya Koti, Judicial Officers lazima wawe wale wamehitimu.

Com. Muigai : Yes.

Mr. Mohammed Abdulkadir : Na pia Judicial Officer lazima awe... isiwe ana andikwa na Rais. Aandikwe na Judicial Service Commission peke yake. Na mtu yoyote ana fanya kazi ya Judiciary asipitishe miaka thela... hamsini-na-tano kama kawaida ya watu wengine. Asiwe watu miaka sabini, sababu kuna watu wengi sana wanakuja ku... wame soma. Na watu... unaskia mtu moja tu ndio anakaa ndani ya Court ya Kenya maisha yao yote. Mimi na ... wakati mimi na sikia kuna mtu, mimi na juu wakati mimi niko standard one mpaka leo iko ndani ya kazi hiyo. Kwa hivyo Judicial Officer must... retirement age yao iwe 55 years. Hiyo ni Judiciary.

Policital parties. Sisi Kenya tunataka chama tatu tu ya kisiasa. Ile ingine yote ni udanganyifu ya Serikali...

Com. Muigai : ...[...uHu!...].

Mr. Mohammed Abdulkadir : Nalipwa pesa, nasema kwenda unda yako, kwenda unda yako, ile wa justify ile upuzi walisema kwa Imf na mahali kwingine. Kwa hivyo sisi tunataka chama ngapi... vyama ngapi, tatu peke yake. Na hiyo chama iwekwe nguvu, na hiyo chama hata Katiba yao sisi wananchi tuandike ile iwe chama ya wananchi na iwe kazi yao ni check and balance ya Serikali. Mtu yoyote anaye pigania... nomination ya chama hiyo hana haki kuruka na kwenda chama hiyo ingine. Ni haramu kama wewe ni Kanu alafu uki anguka kwa mlolongo una kwenda kwa Dp, kama una anguka kwa Dp una enda Ford Kenya, hiyo yote ni haramu.

Serikali lazima ipewe pesa sawa na chama... chama yoyote sawa wakati ya campaign. Kama yeye anampa Kanu shilingi million mia moja, apewe Ford Kenya, iwe chama yoyote ingine, apewe chama yoyote pesa sawa. Sababu chama yote ni ya wananchi. Pia wananchi ya Kenya lazima wathibitishe, wa seme, ako katika chama gani. Uwe chama fulani damu, yaani wewe hapana mtu ya kurukaruka, wewe unajulikana wewe ni Kanu na unakufa Kanu. Wewe ni Dp ukufe Dp, wewe ni Ford Kenya ukufe Ford Kenya, sio wewe unamanga manga, na haribu hata heshima ya chama.

Com. Muigai : ...[...uHu!...]....

Mr. Mohammed Abdulkadir : Local Government. Serikali ya mitaa. Uchaguzi ya Chairman na Mayor, lazima ifanyiwe na wananchi. Mtu yoyote anakuwa Chairman ama Mayor awe na masomo mpaka degree ya university. Sababu tunataka awe na nguvu ya kuendesha hiyo kazi sawa sawa na Governor. Kwa hivyo hatutaki mtu ... machachari ana kwenda kaa huko.

Com. Muigai : ...[...uHu!...]....

Mr. Mohammed Abdulkadir : Pia, yeye ata kaa...ako na mali gani na asset gani atueleze utajiri wake ili tumuamini si mtu wa kupora. Naye awe si mtu ikona mambo ya kurushwa rushwa na mambo ya criminal criminal hii yote. Ikona moral moral na ethical conduct must be good in place ili awe aangaliwe.

Councillors: Councillor yule iko juu na yule anahitaji kwenda kupigania kiti lazima awe form four. Na awesema akona mali gani mbele ya kupigania kiti. Yeye atapigania tu kama Mayor. Two terms ten years sio mtu anakaa miaka yote anakuwa monotonus hatutaki haat kuona wewe. Kwa sababu iko form fours wanakosa kazi na wewe unakaa tu huko peke yako.

Basic rights. Iwe ni jukumu ya Serikali. I propose it is the duty of the state to provide all basic rights these are, I am going to mention a few things. Clean water, basic need food shelter, free education and medical care security and protection freedom of expression, association and movement, religion and assembly. Clean environment, mazingira mzuri na pia haki ya kuajiriwa. Kama hapana ajiriwa mtu hapanapata kazi apewe haki yake awe na siku ya kujilisha mapak wakati serikali itakampatua kazi.

Natural resources: Mali ya asili. Tunataka kupendekeza hivi. Kitu yoyote iko juu ya ardhi hii ni mali ya wale wanaishi hapo. Juu ama chini yote ni mali ya wananchi hapo. Kama ni muhimu kwa Serikali ama company hawa ndio wata kaa na ile investors na waseme sharti yao na waweke na wa kubaliane ili hiyo company ama Serikali ifanye exploration ama exploitation.

Pia napendekeza the management and uses of natural resources. Uchungaji na utumiaji ya mali ya Serikali. Serikali iko na mali gani? Kitu kama tourism, airport, harbour, railways, national parks, public universities, Kenya pipeline and other parastatals. The revenue generated, pesa inatoka kutoka hiyo resources lazima ipelekwe kwa consolidated fund na iwe decentralized at a local authority level. Na uchunganji lazima tubuni national resource commission kitu kama hiyo ili hiyo rasilmali ya Serikali ichungwe na igawanyiwe kwa wananchi vile inawatosha. Na rasilmali ya Serikali isi ingiliwe na chama ana executive ama legislature it should be a free and independent commission.

Uandikaji na uvutaji ya hawa watu ni juu ya hiyo commission na kuna ajabu ingine katika Kenya hii. No retired government officers of any rank should be appointed to either board of directors or executive chairman of that commission or even parastatal for that matter.

Citizenship uraia: Raia ya Kenya mtu yoyote anajua ni nani raia yule anazaliwa ndani ya Kenya ni raia. Yule tunapendekeza kama mzungu na hawa mborana awe automatically ni raia ya Kenya ama kama mzungu mborana au msichana mzungu hiyo msichana awe ni raia ya Kenya. Raia ya Kenya inafaa kubeba nini Passport pekeyake. Kila mwananchi apewe passport sio Id. Na kama wewe unataka zaidi zaidi unataka kujua huyu ni nani pengine ni usiku kila raia ya Kenya awe na pocket constitution kidogo ndani ya mguko yake kila wakati.

Legislature: Mtu anataka kuwa mjumbe hawezi kuwa Minister tunapendekeza zaidi. Waziri asichaguliwe kotoka wajumbe. Hiyo ni yangu maoni. Serikali akitaka kuchagua Minister kutoka sheitani achague lakini sio mjumbe. Kwa sababu waki complain watu amehungwa hata hawa sikii sisi. Kwa hiyo tunataka mjumbe wa national assembly iwe free from executive wasiwe pamoja.

Pia sisi tunataka aina ya Serikali mmoja, mimi binafsi nasema tungependa kuwa na Serikali ya federal state ili tupate rasilmali iwe karibu na sisi. Ile tupate Serikali awe na cheques and balances. Tunataka federal state majimbo ambaye hana provincial administration juu mpaka chini hakuna ndani. Majimbo. Tunataka Majimbo...

Com. Muigai : Zungumza kwa mic.

Mr. Mohammed Abdulkadir : Nasema, mimi nasema tunataka system ya government ambaye ni federal. Federal government itakuwa na chamber mbili katika Parliament, ya Senate na ya National Assembly ya Mp's. Kwa hivyo sisi kama tunapendekeza federal state Senate atatulinda katika regional. Na kama sisi wote ambaye wananchi hawapendi inaletwa na wajumbe Senate ndio ita pigania sisi. Kwa hivyo tuna-propose a federal state. Ile tupate rasilmali iwe karibu iwe inakuja karibu na sisi sasa uki toka kwa kazi unaenda Nairobi. Ukitaka

kuchukuwa Passport unaenda Nairobi. Kama tunapata federal state mimi na fikiri kitu inakuja karibu nasisi hata tunaweza kuwa na regional President. President inakua mbili halafu ile nyingine inastuka. Ama mnafikiri hiyo sio mzuri. Majimbo ni mzuri na mimi nasema sisi tuwe ma Majimbo.

Kwa hivyo ningependa kumalizia hapo kwa sababu.

Com. Muigai : Asante sana. Hussein Abdi? Hussein Abdi? I think we should let them talk ...[inaudible]... now what time do we go for prayers ...[inaudible]... what we can do is break for...

Mzee Hussein Abdilafa : Asalaam- Aleykum! ...[Vernacular through translator]...

Translator : Anasema anaita Hussein Abdilafa ni mkaaji wa Kinna.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Yake ni machache.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Yaani shida inatukabithi.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Tangu ukoloni tulidhulumiwa na pia hata wakati tulipata independence tukadhulumiwa.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Anasema sisi wengine wetu tuko na mifugo na pia hata kama shamba ndogo tukonaye sehemu ya Kinna.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Anasema Kinna sisi tume changanyishwa na wanyama tunaishi katika sehemu ya park.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Anasema nchi yetu ambaye ilikuwa zamani ya malisho imechukuliwa na watu na Angaine.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Hiyo pahali inaitwa Darbachontupi? Ni Angaine amechukuwa.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Anasema ni wakati ya shifta ile sisi tulitoroka kwaajili tulikuwa tunaogopa bunduki na nchi yetu ikanyakuliwa.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Ika fanywa national park leo ambaye mnaona pale Meru, Meru National Park.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Ile iliobaki naye Council ika nyakua.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Sisi watuwa Kinna tukabakishwa sisi nawanyama mandovu.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Usiku na mchana watu na mali wanakufaa, nduvu ina maliza na simba.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Hatuna haki.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Yeye anapendekeza Katiba ya Kenya iwekwe hii Katiba mpya ya kwamba, ndizi yetu moja

ikivunjwa na ndovu shilingi elfu kumi kwa kila mti ya ndizi.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Mtu ambaye atauliwa na nduvo ridhaa yake itakuwa ni million mbili anapendekeza.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Anasema ule ambaye atakuwa ni kiwete labda ameumizwa na amekuwa disabled kidogo kwa ajili ameumizwa na mnyama. Maisha yake yote atakuwa na hiyo disability alipwe million tano.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Hiyo boundary ambaye imechukuliwa na huyo jamaa ambaye amemtaja hapa Angaine anasema turudishiwe hiyo pahali wamenyakua wamefanya Meru National Park.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Kuna pahali inaitwa Duse katika sehemu yetu ambaye maskini yetu wanaishi naye.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Sisi umaskini ambaye walikuwa wanaishi katika sehemu ya Duse leo hatuna haki ardhi ya Duse imenyakuliwa.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Mtu ambaye leo amechukuwa license ya kuchukuwa sehemu ya Duse ni mhindi.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Mzee anasema katiba iseme mhindi huyu aondoke haraka hatutaki kumuona katika ndani ya Duse.

Mzee Hussein Abdilafa : ...[Vernacular through translator]...

Translator : Ni hiyo tu

Com. Muigai : Next to Hussien Abdi amezungumza. Adan Ali Wako? Adan Ali Wako? Adan Ali Wako? Lakini wewe unasaidia sana. Speedy speedy. Kwa hivyo kaa hapo.

Mr. Adan Ali Wako : ...[Vernacular]... Asalaam Aleykum! Mapendekeza yako. Okay kwa jina mimi naitwa Adan Ali Wako kutoka Kinna.

Mapendekezo yangu sasa ni kuhusu sheria sasa. Malipo ya watu waliouwawa na Serikali yao na dhulma wakati ya kijini from 1963 to 1967 hiyo ni moja.

Ya pili mpaka ya Isiolo District iwe ya wakati ya ukoloni ya zakale irudishwe pahali pake.

Ya tatu madini na rasilmali huko chini ya ardhi iwe wa wakaaji ya eneo hilo. Kwa mfano kama Duse hapo.

Ya nne County Council ipewe nguvu zaidi kuliko hii ya sasa.

Uchaguzi ya ubunge na madiwani iwe siku tafauti.

Kuhusu mambo ya Waislamu. Chief Kadhi wetu wa Kenya iwe ikichaguliwa ma Waislamu sio Presidential appointee. Kwa sababu President sio Muislamu hajui sheria ya Waislamu. Ni mzuri sisi wenyewe tukae Waislamu maulamaa wachague.

Waislamu tena tupatiwe wafanyi kazi wetu Waislamu ambaye wanaganya kazi na Serikali nafasi ya siku ya Ijumaa kwa sababu ya maombi yetu. Kwa sababu wakristo wako na siku mbili hapo hiyo siku sio siku yetu. Siku ya Jumamosi na Jumapili sio yetu Waislamu. Kwa hivyo napendekeza mimi siku ya Ijumaa ifanyue siku ya maombi ya Waislamu.

Kuhusu mambo ya National Park vile wazee wengine wameongea hapo. Kuna sehemu zingine ambaye tuko naye hapo ambaye tumenyanganywa na Serikali inaitwa Meru National Park. Hiyo sehemu ni sehemu ambaye imekatwa kutoka kwa sehemu ya Isiolo District na Wameru na upande ingine na watharaka. Hiyo sehemu Serikali hatukupata kutoka kwa Serikali ridhaa. Compensation ndio tunataka. Tupatiwe compensation yetu. Kuna hii. Yaani ardhi sehemu zetu ambaye zimechukuliwa na Serikali hatujapata malipo ridhaa hatujapata.

Ya mwisho kabisa natakakusema hivi. Katika Kotini ama katika bunge wakati yakuapisha ma-ministers ama wabunge kuna kitabu ya Koran zimewekwa pale. Kwa mfano hiyo kitabu kama wewe ni Muislamu unapatiwa na mtu ambaye sio Muislamu. Tunataka hiyo kitabu wakati wakupatiwa mtu yule ambaye ni Muislamu anaapishwa pale ipatiwe kwanza ishikwena Muislamu. ...[Vernacular]... Kwa hivyo hiyo kitabu tunataka yule mtu ambaye anaapisha ama anapatiana hile kitabu awe ni Sheikh Muislamu awe pale halafu kama ni kuapisha yeze mwenyewe aapishe sio Mkristo a shike ama mkafiri mwengine, kwa mfano mwakajana mimi na kumbuka huyu assistant minister wetu wa hapo mjumbe wetu ameapishwa na [?] siambaye hata Muislamu sio Mkristo mkafiri. Kwa hivyo hiyo ni haramu katika sheria yetu. Hiyo kitabu katika Kotini katika hiyo ujenzi ya bunge asiguswe mtu ambaye sio Muislamu hana tahara.

Kwa hivyo nimemaliza mapendekezo yangu hapo.

Kwa moja kuna dhulma hapa kubwa, kwa mfano hiyo ofisi ni yetu ya County Council, mnakuta hapo Eck, Isiolo South Constituency. Hii ofisi ni wa wananchi Serikali ikikuja inatumia watu wa Electoral Commision of Kenya wako na pesa yao ambaye wamepatiwa na Serikali. Unaonawakati ingine pale imepanguswa Moi alipokuja hapo ineandikwa Kanu Office. Mimi mwenyewe ni mshahidi hapo mnweza kuona tu. Pahali imepanguswa imepakwa ile bendera nini ya Kanu ikaandikwa... hii sasa tunataka Kanu wakikuja walipe kwa County Council, Electroral Commission wakikuja kutumia hiyo ofisi walipe kwa County Council.

Kwa hivyo minamalizia hapo. Asanteni sana.

Com. Muigai : Mohidin Ali? Mohidin Ali? Yuko hapa, kabla huja anza useme jina yako tape ichukuwe jina.

Mr. Mohidin Ali : Asalaam Aleykum! ...[Arabic dialect]... Mimi naitwa Mohidin Ali mimi ni kijana wa Garba. Mimi niko na mapendekezo kadhaa. Mimi ni kajana Muislamu na baada ya hayo mimi ni kijana mborana ya kwanza kabisa ni kuhusu Uislamu mimi ya kwanza kile mimi napendekeza ni kutaka sheria ia islamu ituletewe hapa na wale wanatunia hiyo sheria wawe Waislamu.

Ya pili kuhusu vijana sisi wavijana Waborana hakunu Serikali inatugundua, masomo yetu haigunduliwi mimi nataka kusema masomo ya vijana wa Kentya wote wawe sawa. Kabilia gani, mborana, mkikuyu, mkamba wawe sawa.

Zaidi ya hayo mimi kama kijana Muislamu kuna haki ya dini mimi lazima niwe naye katika dini yangu kama nimesoma madrassa na sija soma shule masomo yangu ya madrassa lazima Serikali iangalie. Kama mimi niko na Degree ya Madrassa lazima hiyo Degree Serikali igunduwe vile inagunduwa Degree ya masomo ya shule. Na

kama Degree ya shule yaani akona ofisi Serikali iweke ofisi hasa ya yule mtu ambaye akona Degree ya masomo ya Madrassa ambaye ni elimu.

Baada ya hayo Serikali iweke area hii ambaye ni subdistrict ofisi fulani ya kuangaliwa an independent office. Kama leo mfano Police officer akikuja kwangu hapa au hapa Garbatula nikitaka kupeleka shida yangu nitapelekea officer yake mkubwa lazima an independent office iweke pahali fulani ya mimi kuleta shida yangu. Hakuna pahali mimi nitapeleka shida yangu. Lazima nipeleke pahali ingine. Yaani a Police officer ni peleke kwa officer yake mwengine lazima pahali ingine itengenezwe an independent office.

Com. Muigai : That is one of the best suggestions nime sikia...

Mr. Mohidin Ali : Hiyo iwekwe kwa mapendekezo yangu. Zaidi ya hayo mimi nataka kusema yale yametoka hapa ardhi zetu hapa ikiwa madini ikiwa mazao iwe ni faida yetu sio wengine County Council, Government wakae mbali wakiitiwa na watu wajamii wachukuwe hiyo fursa wakuje. Lakini wasipoitiwa wakae mbali na madini hapa. Iwe ni yetu.

Zaidi ya hayo mimi nataka kupendekeza hivi. Yule mfanyakazi Muislamu awe mwalimu awe daktari Uislamu yake igunduliwe dini yake. Right of religion igunduliwe. Kama niki fuga, Uislamu inahitaji mtu kufuga ndevu lakini Serikali haitaki. Mimi nataka nipendekeze Serikali iweke mzuri Muislamu ambaye ni mwalimu aweke, Muislamu ambaye ni jeshi aweke yule polisi aweke. Tunataka right of religion. Baado hatujawekewa katika katiba iliopita. Kama tungewekea leo hatunge katazwa. Lakini uismalu inataka mtu afuge ndevu. Muislamu inataka mtu avae kanzu, kanzu igunduliwe tuvae kila pahali ofisini. Tunataka katika every institution tuwekewe haki ya religion, right of religion iko lakini hatu tambuliwi. Katika mapendekezo yangy natakakusema iwekwe nainangaliwe vizuri. Zamani ili kuweko lakini hawakuchukuwa. Mimi nataka kusema iangaliwe vizuri.

Mimi nataka kusema mfanyakazi iwekwe ya Muislamu apatiwe serikali ijenye benki maalum ya kuangalia wafanyakazi Waislamu leo Muislamu anateswa anasema yeye hawezi chukuwa interest wengine wanachukuwa pesa hiyo pesa inafaidi watu wao inafaidi vijiji yao inafaidi kila pahali. Lakini Muislamu hana wakati atasema hatachukuwa interest na serikali ijenye benki maalum yakupatie Waislamu pesa ambaye haina ribaa. Serikali iangalie vizuri kuna hiyo haki ya Muislamu na sio Muislamu, ya yule mtu ambaye sio Muislamu.

Mimi ya mwisho nataka kupendekesa hivi. Serikali ya Federal Government mimi napendekeza hiyo serikali. Badala ya hii serikali ambaye tukonaye saa hii.

Zaidi ya hayo mimi nataka kusema serikali isichukuwe, yaani President asichukuwe sheria mikononi mwake vile

zamani walisema the President is above the law. Sitaki kusikia hiyo. Mimi napendekeza serikali, the President should not become above the law. The person who is above the law is the one who creates people, so the President must be under the law.

Zaidi ya hayo mimi nataka kusema wabunge wachaguliwe kutoka wale ambaye wamesoma form four. Lakini sio wale ambaye hawakusoma. Councillor naye wakuwe wenyewe hivyo. Wale wanesoma form four.

Zaidi ya hayo mimi nataka kusema County Council ipatiwe nguvu. Mayor ya County Council apatiwe nguvu ama yule amekaa co-ordinator ya County Council apatiwe nguvu zaidi kuliko ile wako naye leo. Wanaamurishwa na watu kutoka mbali wawe na nguvu katika hiyo County Council.

Mwisho kabisa mimi nataka kusema serikali leo Rais ya Kenya akisema emergency fulani ya watu ifanyiwe leo serikali itachukuwa hiyo hatua haraka iwezekanavyo. Rais akichukuwa mkononi sheria ya kusema watu kabilia fulani, wa malizwe nasema serkali wata maliza. Hiyo ni sheria imewekwa. Hiyo sheria itolewe kabisa.

Mwisho kabisa nataka kusema ya wale wanavaa wanawake Waislamu, wasichana Waislamu wakubaliwe kuvaahila wanayoitaka kama ni nguo kuvaahila mavazi mazuri wavae ofisini katika kila pahali hiyo nguo yaani sio kimila that one is not a culture but that one is a law let people know that that one is a law in the new constitution.

Kwa hayo nasema Asalaam Aleykum! ...[Arabic dialect]...

Com. Muigai : Asante sana, Asante sana. Huka ali Hassan? Hassan Ado? Boru Ali? Namna hiyo muje haraka haraka. Tuanze na Huka Ali? Dakika mbili mbili mbili. Huka Ali?

Mr. Huka Ali : Asalaam Aleykum! Kwa hivyo...

Com. Muigai : Haraka haraka tafadhali

Mr. Huka Ali : Kwanza maoni haya. Jina Huka Ali. Huka Ali. Mapendekezo haya...

Com. Muigai : Na bwana Ali kwa vile umeandika maandishi yako vizuri ufanya summary tafadahli

Mr. Huka Ali : Mapendekezo haya ni mengi na mi mapendekezo ya jamii mzima kwa hivyo tume gusia sehemu nyingi na sehemu hizi zote ni muhimu na inagusia labda maisha yetu ya kila siku. Kwa hivyo mtaniomba radhi ingawa itakuwa kwa ufupi kugusia kidogo kidogo.

Kwanza ya Constitution supremacy yaani jinsi ya kuimarisha katiba hii tulisema ya kwamba Parliament should not have powers to amend any part of the Constitution. Mambo haya ambayo tunarekebisha bunge isijaribu labda ku badilisha bila labda kuarifiwa na wananchi ambayo wameleta maoni haya.

Sehemu ambazo labda zina husu dini katika katiba hii mapendekezo maoni ambayo yanayo husu dini yasijaribu kubadilishwa kwa haraka haraka bila labda ithini ya wananchi. Kama labda yatabadilishwa yarudi kwa wananchi kwanza through referandum tena.

Citizenship: Wakenya, nani atakuwa ni Mkenya vile tunavyo ona mtu kutoka sehemu hii Muislamu ama mtu kutoka dunia akitaka kupata passport labda anataka kuenda Pakistan. Mtu kutoka sehemu hii anasumbuliwa anachunguzwa anaulizwa maswali mingi. Huku labda Njoroge akikuja, Njoroge huulizwa maswali fupi. Kwa hivyo katiba hii katiba tunarekebisha sehemu hii labda katika sector ya Id mtu asiwe screened asisumbuliwe sana.

Tena Rais the President should not have powers to withdraw citizenship of Kenyans. Rais asipewe jukumu labda ya kuchukuwa ithini ya Mkenya aseme huyu mtu sio Mkenya. Mtu anaishi hapa wote ni Wakenya Rais asipewe mamlaka ya kuchukuwa citizenship ya Mkenya bila ithini yake kuhusu jambo hilo.

Tene tunapendekeza juu ya citizenship double citizenship of a Kenyan should be guaranteed should be encouraged to allow Kenyans to live or work in any part of the country [world]. Wakenya mimi nikiwa Mkenya sasa naweza kuwa raia ya Kenya ama raia wa Ethiopia. I should have two passports. Hayo ya pitishwe.

A Kenyan citizen should have protection of lives and property and have freedom of worship. Kila Mkenya lazima ana haki ya kupata malikuwa na malikuwa na uhuru ya kuabudu na uhuru ya kuongea. Hapa leo kunamatatizo mengi katika hii sector.

The Defence and National security tuna mapendekezo mingi lakini labda hapa kama moja mbili. Tune sema ya kwamba the President should not be Commander in Chief of the Armed Forces and the Executive should not have exclusive powers to declare war. Instead the public should declare war through referendum. Hapa leo vile tunavyo ona Rais Moi ndio Mkuu wa Amri Jeshi. Tunapendekeza ya kwamba Raisi atakaye kuja katika katiba itakayo ikuja asiwe labda Mkuu wa jeshi. Kuna wengi wana tosheleza hiyo kazi. Tunasema the President awe asiwe Mkuu wa Amri Jeshi. Na kama hivyo napendekeza basi maoni ya Raia ichukuliwe that is referendum.

Parliament should appoint / nominate the Commander of Security service. Yes. Watu hawa katika ulinzi iwe ni hali ya shughuli yaani ni kazi ya bunge kuteuwa ma-officer wa ulinzi katika hiyo sector.

Parliament should make laws for the Armed Forces and establish court martials to execute them such as a system of government.

A system of government Federal government should be adapted with the Prime Minister running the affairs of the state and the President remaining ceremonial.

The Deputy Prime Minister should be a Muslim in the coming Government.

Com. Muigai : Why not the Prime Minister himself?

Mr. Huka Ali : The age requirement for a president or a prime minister should be 45 years and above. Anayetaka kuwa Rais awe amefikisha umri ya miaka arobaine na tano katika Katiba inayokuja tunapendekeza hivyo.

Age requirement for an Mp should be 30 years and above. Mtu akitaka kupigania kiti cha bunge awe amefikisha takriban miaka thelathini. An Mp or any candidate vying for a post should be a degree holder. Mtu anayetaka kuwa mbunge awe ni msomi halisi awe amefika katika chuo kikuu na awe ni mtu ambaye ana degree.

Com. Muigai : ...[inaudible]...

Mr. Huka Ali : Any person vying for the post of Mp or a Prime Minister or President must be a Kenyan citizen. Yeyote atakaye pigania, wadhifa wa Mp, waziiri mkuu ama rais awe ni Mkenya kamili. Concept of nomination should be encouraged but special preferences should be given to the minority groups. Yaani mbunge maalum, ama mbunge maalum iendelee. Mtu akiteuliwa, shughuli za kuteuwa wabunge maalum iendelee lakini iangaliwe vizuri, labda minority groups, blind and what have you. Watu hawa wawe wakiangaliwa.

The salaries of the Legislators should be determined by the general public through a referendum. Hapa vile tunavyo ona wabunge, hakuna anayejali wabunge wanapata mshahara namna gani. Hivi karibuni walijipatia asilimia mia nne, huku waalimu wanataka mshahara lakini wana katazwa. Wabunge wasijipatie mshahara Wabunge wasijiongezee mshahara wale wataangalia haya maoni yawe ni through referendum. Maoni hayo, kura ipigwe na wananchi waamue kama... kama wabunge wataongezewa pesa kiasi gani, ama wa katazwe. Salaries and Benefits of the Legislators should be in line with other less developed countries bearing in mind the economic situation of the country.

Executive: Sasa hii ni sector ya Serikali, Rais akiwa kiongozi, waziri hapo. Tulusema ya kwamba sehemu hii ni muhimu sana. Hii ni sehemu ya Serikali, hapa in charge ni Rais. Chini yake iko mawaziri. Hapa tuna maoni haya, ni mingi lakini, vile nime sema. Nitasema machache. An executive should be a degree holder, an executive should be upright and God fearing or either practicing a religion. An executive should declare his wealth through the Kenyan Gazette. An executive should have an important post before becoming a Legislator.

A Prime Minister should have the following important duties amongst others. Appoint his ministers, another assistant another assistant, appoint diplomatic corps, appoint attorney general, chief justice ...[inaudible.]... chief kadhi should be a member of the Executive representing Muslims. Tumesema ya kwamba Chief Kadhi awe member of the Executive. Awe kama, katika Bunge, awe kama Waziri, huko juu. Hii sector ya Executive ndio muhimu sana. Hii ndio Serikali. Chief Kadhi awe katika Executive.

Kadhi should also become an ex-officio member of Parliament. Leo licha ya wabunge wengine tuko na Attorney General, Speaker ambayo wako katika Bunge kila wakati. Attorney General ni mkuu wa sheria. Yeye si mbunge. Kwa vile Bunge ndio ina... ina... ina... tengeneza mambo ya... mambo ya... mambo ya sheria, Ag ana kuweko ndani. The Speaker pia ni ex-officio. Tuna thibiti... tuna... tuna... pendekeza ya kwamba, Kadhi should also be an ex-officio as ...[...?...]... Waislamu awe ex-officio kwa sababu Kiislamu ina sheria yake. Kwa hivyo ati awe katika nini, katika Bunge, katika... aweke an ex-officio of Bunge.

Attorney General should go through suspects files and convicts files and give judgment on appeal. Should no be biased in executing his duties. And should not be manipulated.

Judiciary: Hii sehemu pia ni muhimu kwa sababu ina husu... ina tuhusu sana. Islamic Courts should be introduced to serve Muslims both Civil and Criminals. Koti ya Waislamu lazima ifunguliwe kuhukumu... kushughilikia Waislamu. Muslims should be judged according to the teaching of the Koran. Tunapendekeza ya kwamba Waislamu, waadhibiwe kulingana na Koran. Kwa sababu Koran ina husu kila sector ya binadamu, na hakuna kitu ambacho kimewachwa wazi. Muslim Judges should be employed to handle Islamic labour matters. Judges wa Waislamu waajiriwe, ili wajaribu kushughulikia, shughuli za Waislamu. Islamic Law Schools should be established.

The special cells and jails should be put in place for the Muslim convicts clothing and room for prayer should be there. Hapa tunesema ya kwamba, jela kwamba... kama ni wafungwa, Muislamu yuko tafauti na Wakenya wengine. Kwa sababu Waislamu ana taratibu zake za maisha. Ana vile anavyoishi, Muislamu lazima awe safi. Majela mengine si safi kwa Muislamu, Muislamu anatakiwa asali na kila wakati asome Koran, anatakiwa anaenda zake Kotini. Kwa hivyo tunapendekeza cells, special cells for Muslims should be opened.

The Chief Kadhi should be head of the Islamic Judiciary and should work independently. Tumesema ya kwamba Chief Kadhi apewe nguvu za kutosah ili aweze ku... kuongoza Waislamu kote nchini. Awepe nguvu ajaribu kupendekeza shughuli za Waislamu bila uwoga ...[inaudible]... Apewe uhuru. He should be independent. Serikali isijaribu kumuvuta vuta hivi. Leo katika Bunge Serikali ina vuta mtu. Serikali isi vute mtu.

The Chief Kadhi, another Kadhi should be appointed by a body of Muslim scholars. A body of Muslim scholars ...[Arabic]... should be established by the Muslims. Tumesema ya kwamba kikundi hiki cha ...[Arabic]... kibuniwe. Kikundi hiki ambacho kina jaribu kuhusika na Waislamu, ki... ki... kibuniwe. Na kikundi hiki ndicho kina jaribu ku... kuhusika na kila... na kila swali ...[inaudible]... juu ya Waislamu. [All should Kadhis should be tried?] by the ...[Arabic]... in case of misuse of office or inefficiency. Hapa tumesema Kadhi basi yuko chini ya nani, ardhi... I mean Chief Kadhi, I mean Kadhis should be under this. Wale wako chini ya ...[Arabic].... ...[Arabic]... ndio inaangalia taratibu, tabia, na kama huyu Chief Kadhi ha fanyi kazi lazima hawa ndio wataadhibu yeye.

Basic rights... haya yametajwa hapa awali, lakini kuna mambo tumesema. People with disabilities should be given special treatment, eg., food, shelter and the rest. Hapa kugusia haki za binadamu, tumesema ya kwamba wale walemavu, walemavu nchini Kenya hawaangaliwi. Walemavu wapatiwe haki ya kutosha. Kama vile chakula, malazi bora na mahali pa kupumzika. Walemavu yaani disabled people should be given special attention on food, sheltering and other areas. People with special disabilities completely blinded and wheelchaired should not be sentenced or fined.

Hapa tumesema watu ambayo... walemavu. Mtu ambaye hana miguu, labda hana macho yote mawili, watu hawa wasi pelekwe Kotini. Wanashida zao wenyewe, ni maskini tayari, hana miguu miwili, hana macho mawili, hana mikono miwili, mtu huyu asishtakiwe awachwe tu, awachwe huru, akae. Special homes should be established for mad and psychiatric cases. Hapa Kenya tunaona shughuli za walemavu ama, wale ambayo vichwa vyao si sawa hakuna wanaojali hawa watu. Labda centers zifunguliwe, watu hawa waangaliwe.

Land: Pastrolists land belongs to the community. A board of trustees should be chosen from each division of the district, three people from each division. Mambo ya lands tumesema ardhi ni ya wananchi, na katika kila tarafa watu watatu wa chaguliwe. Na hao ndio wata simamia maswali juu ya ardhi. Pastrolists communities should be confined within the grazing blocks established in the colonial boundaries for the purpose of eradicating cattle rustling, livestock diseases and over grazing. Tumesema ya kwamba wafugaji wote wanamipaka zao, kila kabila kutoka wafugaji wakae katika sector zao, boundaries. Kwa sababu utulivu wa kutokuwa na amani ulinzi huletwa na mchanganyiko wa watu hao. Kwa hivyo tunapendekeza wakati ya colonial era kila jamii iko na boundary yake. Kwa hivyo Serikali itakayo kuja ni lazima itie mkazo zaidi, jamii yote wawe katika sehemu zao.

Barazaa ya Wilaya, ama local government. mayors and council chairmen should be directly elected by the people, and should serve for a five year term. Haya yametajwa hapa awali. A Councillor should have an ordinary level of education and above Division III or D⁺ in 8-4-4 system. Yaani anayetaka kuwa Diwani, lazima awe ni na... ni msomi kiwango fulani. Amepata daraja la tatu ama katika mfumo mpya wa nane-nne-nne awe ame pata D⁺, hayo ni kurahisisha kazi. Leo hii tunaweka mikono ya kwamba mabaraza yote nchini kuna matatizo. Kwa sababu madiwani wote si wasomi. Kwa hivyo wakisoma tuta kuwa na matatizo machache.

A nomination of a Councillor should go to special groups eg., women, blind, crippled, and minority groups. Hapa vile tunavyoona leo, mtu akiwa ame... amekuwa nominated imekuwa siasa. Mtu anapatiwa hiyo udiwani labda mtu kutoka kama ni siasa uko fulani, hii kazi... hii nomination of councillors has a purpose. Iko na sababu. Ingawa serikali haifuati. Imebuniwa kwa sababu labda, wale jamii ambayo hawaja bahatika kama walemavu, watu ambayo ni wachache katika hiyo sehemu, wa patiwe nafasi. Kwa hivyo pia iangaliwe, tumesema.

An aspirant should be twenty-one years and over, for a councillor and thirty years for a mayor.

Anti corruption units should be identified with frequent and be arraigned in court, that is. Anti corruption units identify Council with frequent, and be arraigned in court. Wale wana husika na labda mambo ya ufisadi sector hiyo iangalie ya kwamba Council ambaye iko na shida wa angalie na washike wanahuksika, na wapelekwe Kotini mara moja. Their books of accounts should be inspected after every six months. Tunaona ya kwamba, Council iko na pesa ingine, lakini pesa hizo za raia, zinatumwiwa vibaya. Kwa hivyo serikali itakayo buniwa ichunguze zaidi, ya kwamba pesa hizo, zisitumiwe vibaya na watu wachache.

Livestock: Sehemu hii ni muhimu sana. Sisi ni wafugaji. Livestock... mambo ya wafugaji. A livestock market should be established within the areas of grazing. Hapa tunahitaji soko la wanyama, labda factory ya nyama, mambo haya yabuniwe hapa ili sisi tuweze kuuza wanyama wetu hapa. Badala ya kupeleka wanyama wetu Nairobi. Wanaotaka kununuwa ng'ombe zetu, mambo mengine wote wakuje hapa. Sisi tusi peleke ng'ombe zetu Nairobi. Factories for livestock ...[inaudible]... should be established. The state should boost livestock sector economically so as to increase its contributions to the Exchequer.

A Board of Commissioners should be set up, and the members should only be pastoralists because they know our problems better. Hapa leo tunaona ya kwamba, Mjalo ndio board member wa mambo ya ng'ombe, Mkikuyu ndio board member, Mkisii... na mambo ya ng'ombe. Kwa nini sisi wafugaji, ni sisi Waborana tusiwe board members wa hiyo sector, ili tuweze kufanya kazi yetu. Tunasema ya kwamba Board ikichaguliwa wafugaji wenyewe, kama ni Wasomali, Waborana, Wasamburu wawe ni Board members badala ya kuweka Njoroge akina Kamau, Otieno

wanakaa Nairobi....

Com. Muigai : ...[...ha Ha! ha...]....

Mr. Huka Ali : The state should only buy the product of our animals and not import from other countries when we have ...[inaudible]... The Livestock the livestock and their products should be advertised in the media. Leo tunakuta ya kwamba Serikali inasema ya kwamba, uti wa mgongo ya Serikali ni majani na kahawa. Jambo la kusikitisha kwamba ng'ombe wetu, wana nyama, wana ngozi, ata mifupa yenyewe, inatumiwa kwa kutengeneza gum. Lakini Serikali inatangaza majani, America kwa Tv kwa media. Kahawa ya Kenya ni bora, ng'ombe yetu pia ni bora kushinda majani. Sindio. ...[inaudible]...

Com. Muigai : ...[...uHu!....]....

Mr. Huka Ali : Kwa hivyo hayo yote ni dhalma tunafayiwa. Serikali advertise, sisi Waborana kwanza tuna ng 'ombe bora zaidi kushinda kila mtu. Ng'ombe wetu ni maridadi sio ...[inaudible]... Kwa hivyo waangalie hayo mambo. The Borana Bulls are the best, I suppose.

Good transport and communications should be set up for easier running of these activities and marketing. mawasiliano bora ya buniwe. Labda tukipata factory hapa ndani ya nyama, ya nini tunataka mawasiliano bora. Barabara zetu zipigwe lami. Barabara... barabara zetu kutoka miaka nne... miaka arubaini iliopita hata hakuna... hakuna sehemu zimepigwa lami. Kwa hivyo katika Serikali zijazo tunataka mawasiliano bora. Kisumu barabara. Mambo kama hii.

More funds should be allocated to the Ministry of Livestock for better health care of our live... animals. More pastrolists should be trained as livestock officers and sent to the localities. Foreigners don't have efficiency in rural areas. Leo tunaona kama hamujui Garbatula leo iko na Officer ya Maji, iko na Officer ya Ukulima, ina Officer ya Veterinary. Lakini wana kaa wapi, urban centers. Kwa sababu hata mkubwa... mkubwa pia ni Mmeru, ni Mjalu, mbona wasikuje hapa ili wajuwe mambo ya mifugo. Kwa hivyo tunapendekeza wafanyi kazi wa ukulima sana sana Veterinary Officer should be stationed around. Locals. Wale wengine kutoka nje, they have proved to be inefficiency, in most cases.

The State should let... should set up savings and credit interest free banks in Muslim pastoral areas. Tumeona ya kwamba wakulima wako na banki yao. Ukienda Meru utakuta, a very big bank. Meru co-operative bank, sisi pia kama wafugaji, katika Serikali itakayo kuja tunahitaji banki ya uko... ya wafugaji, au namna gani. ...[inaudible]... Yes tunahitaji banki ya wafugaji. The State should provide legitimate funds to the owners of large herds of

animals for protection against rustling. Hasa kuna mtu alisema more dams and boreholes should be put in place for animals. Serikali ijenge ibuni, dams ya maji, ichimbe visima vya maji ya kutosha, kwa sababu hapa kila miaka, idadi ya wanyama inaongezeka.

Lakini tunakuta wakati mwingine, kuna majani, lakini hakuna maji. Kwa hivyo tunapendekeza Serikali ijaribu kutupatia sufficient water for our livestock. In case of drought predictions, the State should look for new markets for our livestock outside the country. Wakati mwingi, wanyama wetu wanakufa kwa sababu wananchi hawana suluhisho. Kama nchi zingine katika dunia, Serikali lets say, wakati wa calamities, kama drought inakuja, Serikali will predict ya kwamba, mwaka huu mvua ni mbaya, hakuna mvua, kwa hivyo, wana nini. Wajaribu kununuwa wanyama wetu wote in our ...[inaudible]... pesa za kutosha, badala wewe unaangalia ng'ombe mia tano wanakwisha na wewe unakaa hapa huna suluhisho. Serikali iwe na suluhisho. Iwe na suluhisho wakati wa drought, wakati wa mvua mingi, pia. Kwa hivyo ili waweze.. wananchi waweze ku... sijui kile tutafanya. Yes. ...[eee]...

Elimu: Sehemu hii pia ni muhimu sana, na malizia, tafadhali, mniweradhi kidogo. Elimu. Hapa tumesema ya kwamba, education should be compulsory to every Kenyan should have six... every above... above... above six year. This should also include the religious education. Both ordinary and family education should be free for every Kenyan. Elimu iwe, ni elimu ya msingi, ama ya secondary iwe ni elimu ambayo ina... Serikali ipatie free for ...[inaudible]... University and other colleges should be opened in pastoralist areas. This is to boost education levels of the minority. Hapa ni jambo la kusikitisha kuona kwamba tangu tupate uhuru, hakuna vyuo vyovyyote vya waalimu ya... ama sector ingine kama... kama afya. Hakuna.

Kwa hivyo hii tunapendekeza, hiyo cultural institutions, universities. For example, kama Serikali haiwezi ku... kuhusika na Garbatula High School, Garbatula High School is a big institution. Should be turned into other the colleges ama universities ...[eee].... Kwa hivyo tunapendekeza, vyuo vya waalimu, ama vyuo vya hapa medical centres vibuniwe katika hii sector, kwa sababu, kutoka Isiolo mpaka Moyale amapaka Mandera hakuna vyuo vyovyyote ya... ya... ya waalimu ama ya... labda Garissa tu moja, na hiyo sio yetu. Kwa hivyo tunapendekeza hivyo pia. Schools equipment schemes, equipment schemes should be revived.

Zamani kile kina itwa equipment schemes, wakati Serikali inapatiana kalamu, vitabu kwa kila mtu. Hiyo irudishwe, kwa sababu ni gharama kubwa kwa wazazi. Serikali ilete hiyo scheme. Yaani kununuwa vitabu, kalamu, ruler all these iwe ni shughuli ya Serikali. Sana sana in rural areas, hiyo kitu ifanyiwe. Minority groups like Muslims and pastoralist should get a lions share of education resources. Tunasema hapa Serikali kila mwaka, sana sana mwezi wa sita ikifika, kuna Budget, lakini tunashangaa kama makadirio ya za hizo pesa, zinafika sehemu zetu.

Budgets of Kenya... of Government actually. The Ministry of Education should reach these areas, even these

rural areas. Hakuna senti ya budget ya elimu ina fika sehemu hii. Kwa hivyo tunapendekeza, the budget in the education sectors should reach these areas. Then tunapendekeza, the old system of education, 7-4-2-3, should be adapted. 8-4-4 has proved to be fruitless. Tunapendekeza ya kwamba mfumo ya zamani ya elimu ya saba-nne-mbili-tatu, irudishwe kwa sababu that system has specialization. Leo hii katika mfumo wa 8-4-4, mtu is said to be a master to every thing but jack... jack of all trades but master to none, in 8-4-4, wewe ni kama tu mtu ambaye hana macho, hujui ya kwamba itakuwa nini. Serikali, this is a [?] method and this education is far below, 'C' level in regardless to world education sector. Kwa hivyo tunapendekeza, katika sehemu yetu hii, in the whole system 8-4-4 itupwe mbali, kwa sababu ni gharama mingi kwa Serikali pia wanafunzi wao wanakataa, na vile vile ni mzigo, kwa wananchi. System ya zamani 7-4-2-3, ...[...?...]... irudi, hiyo ni elimu ambaye iko na nguvu zaidi.

Teachers should be paid better than civil servants because they have a delicate task or transforming our children?.

They have more work than any other workers in the state. Tunapendekeza waalimu, sana sana katika sehemu hii, wapewe mshahara ya kutosha. Kwa sababu hao, wanajukumu kubwa katika ujenzi ya taifa hili. Teachers should be well balanced throughout the country. Waalimu wanapogawanywa wa tumwe katika pembe zote, za Kenya hii kuwa usawa. Leo tunakuta kwamba, kuna wilaya ambazo ziko na waalimu wengi. Licha hii yetu. Kwa hivyo tunapendekeza, teachers should be fairly distributed, sana sana in rural areas.

Madrasa education should be recognized. Its teacher training set-up and the teachers paid by the state. Hapa tunasema ya kwamba waalimu wa Madrasa pia, wana husika... wanahuksika sana katika ujenzi wa Madrasa. Kwa hivyo waalimu wa Madrasa wanaelimu. Serikali wanasesma... wanaambia a Sheikh mwenyewe ati he is illiterate. This person is so learned because he has... because he has mastered the whole Koran. This person is not illiterate. He should be... he should be written as a person who has his modern education. Kwa hivyo huyu lazima apewe hivyo. Many boarding schools should be set up for nomadic children. Many boarding schools should be set up for nomadic schools... children ...[inaudible]...

Environment and natural resources: Wakati nafikiri umenipata vibaya, nita jaribu kusema moja moja. Environment and natural resources. Pastrolists grazing land should be community lands and not trust land. Living standards... okay...

Tourism: The state has to provide enough security for tourists. The state should improve transportation and communication for the tourists. More tourist centres have to be put up in place, infrastructures to be improved. The state should improve international relationship for tourism sector and groups. Wildlife should be protected against poachers, should be protected together with their grazing areas during times like film shooting, in parks. Nafikiri nita maliza hapo.

Com. Muigai : Asante sana. Hassan Ado. Na ujaribu tafadhali... ujaribu ku... fanya haraka haraka... tafadhali.

Mr. Hassan Ado : ...[Arabic]... Nafikiri yangu sio mingi wala sio chache. Na nita ...[inaudible]... nita pitia pitia, haraka. Yangu ya kwanza, ni ya Kadhi. Jina ni Hassan Ado. Kadhi. Napendekeza Kadhi achaguliwe na ...[Arabic]... sio Serikali wala sio mawaziri. Kwa maana hawajui Kadhi anatakiwa nini. Kadhi kama tulikuwa... wengine wame zungumza juu ya rais. Kadhi ni rais ya Kiislamu. Na apewe Kadhi nguvu kubwa zaidi, power kubwa zaidi ya kuhukumu. Kwa maana power yeye ana hukumu naye ni power kubwa ambaye imetokana kwa uwezo ya mwenyezi Mungu, Koran tukufu. Kadhi anahukumu kila jambo. Anahukumiwa na Judge, ana zaidi ya Judge. Anaweza kuhukumu chochote kinachotendeka kwa dunia hii. Kwa maana mwenyezi Mungu amesema ya kwamba Koran ...[Arabic]... mwenyezi Mungu ame sema Koran ni hukumu ambaye ilio pita, na hukumu ambayo inangojea wale hawajafika. Kwa mithali Kadhi hawezi kuhukumu hii kidole, ikikatwa ama ikifanywa chochote. Kadhi ana hukumu ...[Arabic]... hii, hii moja kwa moja. Iko katika ...[Arabic]... ya Koran tukufu. Kwa maana inapendekeza hukumu ya Waislamu ...[Arabic]... ya Waislamu wa rudi chini ya Kadhi. Na Kadhi ichaguliwe na ...[Arabic]....

...[Arabic]... ina zungumzia kwa ...[Arabic]... kwa wale ambaye wana fiiwa. Kama vile mama moja alikuwa amepitia asubuhi. Mama ikiwa bwana anawacha yeye. Bwana ana agaa. Ninaomba... ama ninatoa maoni ya kwamba mama huyo, ikiwa yeye ni mfanyi kazi ya Serikali, apate ruhusa wa mwezi nne na siku kumi. Muda ya huzuni. Na sheria yetu inakubalia kuolewa kwa baada ya siku... mwezi nne na siku kumi. Ninatoa maoni. Akiwa mfanya kazi ya Serikali, inakufa nabibi inabaki. Asiteswe hiyo mwanamke. Na asiangamizwe mpaka yeye apate... asiolewe mpaka yeye apate haki ya bwana yake. Huyo hapana fungwa pamoja, katika Koran. Bibi aki maliza ...[Arabic]... yake aolewe na mtu yeye anapenda. Kwa maana tunaona mengi bibi aki... bwana akiaaga mwezi huu ...[Arabic]... aki malizwa na Mama huyu amezaa, wale family ya bwana na ya bibi, na family ya bwana mara ingine hapana sikilizana wanangojea huyu mama aolewe. Akiolewa hapati haki ya bwana yake. ...[inaudible]...

Ninatoa maoni, maoni yangu iwekwe katika Katiba, mwanamke Muislamu... ana fiiwa akimaliza ...[Arabic]... yake ya siku... miezi nne na siku kumi aolewe.

...[Arabic]... likizo ya wakati ya wakina Mama wanajifungua. Wakina Mama wa Kiislamu sheria yetu haikubali, mtu azae kiasi kadhaa. Azae wawili ama azae ka... watatu, alafu afanye family planning. Family planning. Nina toa maoni yangu hiyo kitu iondolewe kwa Waislamu. Wanawake wetu wazae, wanawake Waislamu hataikiwa mwenyezi Mungu anampa hata ishirini malisho yao, sio juu ya binaadam. Wala sio juu ya Serikali. Ana lishwa na ...[Arabic]... Unasikia sasa ya kwamba wa kina Mama waki jifungua zaidi ya watatu hapati maternity leave. Nataka hiyo iondolewe.

Kutairisha wasichana: Unasikia sasa, ina kataliwa na dini yetu ina kubali. Naomba Katiba ya sasa ikubaliwe, na vile itafanya, itegemewe Kadhi ya Waislamu. Kuweka ndevu kwa wafanya kazi. Ndevu ni ...[Arabic]... muhimu sana katika dini yetu ya Kiislamu. Ikubaliwe kuweka Muislamu yoyote, a weke ndevu. Iko wa vijana yetu ambaye wanataka ku andikwa askari au ma-chief, hawatakiaitaki, kwa maana ana mambia nyoya... nyowa... nyowa ndevu. Dini yetu hapana. Ninatoa maoni ya kwamba, Waislamu wa wachiliwe, wapewe ruhusa ya kuweka ndevu. Lakini sio masharubu.

Ruhusa ya Ijumaa ikubaliwe kwa Waislamu. Ijumaa ni siku yetu ya ibaada. Leave ya wafanya kazi wakati wa Ramadhani iwekewe katika Katiba na ikubaliwe. Haswa wa Waalimu wako na taabu sana. Waalimu Waislamu, washule.

Wachinjaji ya mali. Wawe chini ya Imam ya town ...[Vernacular]... kwa maana tuli si... pata kwa radio ama kwa Tv ati Kenya hii ata tuli... watu binadamu wamekula hata nyama ya mbwa, na wamekula nyama ya... ya... ya... punda. Waislamu wako kila mahali. Mapendekezo yangu, kila miji, mchinjaji, waweke chini ya amri ya Imam. Sio ya Kadhi, Kadhi hapana iko katika kila town.

Dini yetu ya Kiislamu isipatetisho. Isitishiwe dini ya Kiislamu. Kuna vitisho. Uki sema kweli kwa sasa kuna vitisho. Dini yetu itambulike kama dini ingine. Dini ya Kiislamu.

Bank: Bank kama vile wengi wetu labda wamepitia. Tuwekewe Bank ambayo haina interest. Interest ni kitu... mkisikia hata Waislamu wanachukua, lakini interest ama ribaa sio haramu ndogo. Ni haramu kubwa, Koran ya mwenyezi Mungu inasema ya kwamba. Kidogo ya dhambi ya ribaa, ni sawa na mtu ana fanya mama yake bibi, ama mtu analala na mama yake. Kwa hivyo Kiislamu kuchukuwa, hata wale wana chukuwa, hata wale wanachukua hawawezi kufaidika. Na wengi wanaogopa hiyo ajili ya interest hiyo. Tunaomba hiyo ikubaliwe.

Bar isiwekwe katika miji ya Kiislamu, ama hii miji majority yake ni Kiislamu, Bar, isikubaliwe, biashara ya Bar. Bar hatutaki ndani nchi ambayo majority yake ni Waislamu. Kama sasa Garbatula. Hatukubali.

Saa inanifupisha sana, nita wacha hapa. ...[Arabic]...

Com. Muigai : Asante sana. Boru Ali. Boru Ali. Karibu Mzee.

Mzee Boru Ali : Asalaam Aleykum Warahmatullah Wabarakatu, aallenii Booru Alii jeedani [inshaallah] dhuub,

Translator : Mzee anasema jina yake anaitwa Boru Ali Mzee wa Garbatula wa msikiti.

Mzee Boru Ali : Alhamdulilah, tiiyy dhuubba, Biismillah Rahmani Raahim, eeh raabbi faahamuu nuu kheen, Aamm dhuubbaa, kwaanzaa mooni aarm ghaadh duumnee, haagg booru dhiiramaa dhuubacuma jirrani, wooni nuu gaadh duumnef mooni. Moonin tiyya taa kwaanzaa qaarra, nuu isiilla - Isiillanii waan issillani feed fed, waan issilaamadhiin qaabdh feed, ukuunki teen taa issilanaa wooni nuu ukumaan woraanaaf aadhiis rasulah adhiqaalamun [inaudible]

Translator : Mzee anapendekeza ya kwamba, anasema sisi ni Waislamu. Na Waislamu tunasheria yetu ambayo inatokana na Koran ...[Arabic]... na hadithi ya mtume ...[Arabic]... tuhukumiwe na sheria yetu ya Kiislamu.

Mzee Boru Ali : Dhuubbin tiyyaleen taa laamesoo woonii ann itti gaadh aanz, isiillanii waan keenyaa faakata, khaa keenyaa khee jiirraa, khaa maaqaan issa issilanaa issilaan took caallaa taauu feen, khaa issilaanii laam intaatiin. [inaudible] Issilaani yoo tookoo maaqqaa qqaabba, issilaan suun maaqqaa issaayyu Laailaaha-Illillaa jeet khaa issilaanaa jet khaa issilaanaa maaqaan khankhee woorria jeedaani, muukaanzuu cuufaale khaa nuurra fuudaani

Translator : Anasema leo sisi Waislamu, ni Kiislamu imetufanya... imetufanya sisi Waislamu tuwe na umoja. Leo jina tunapewa kuliko kuitwa Waislamu, tuna itwa Wariaa. Hii jina Wariaa iwachwe. Katiba iondoe. Isitusumbue nayo.

Com. Muigai : ...[...uHu!...]. . .

Mzee Boru Ali : Waan laammesso ammaalee nuutii gaadh dhaaraan, yoo booraan took khaa dhuubbat khaan issilaanaa aarggan {aarraaraa} issillaan siyyassa qaalii khaan jeedanii, hoojja suun haatua nuut fuudaat maataa irr nuu eejaatanii, diibb suunilee siirkaalii keenyaa khaa nuuraa fuuduu

Translator : Anasema leo Waislamu wakitoa sauti yake, hata mtu moja asimame atetee haki ya dini yake, anaitwa Waislamu wenye siasa kali, nataka leta vurugu hapa. Hiyo tatizo... kutishwa kama hii, iondolewe kabisa. Katiba yetu itulinde ili, tusichukuliwe kama si watu ni watu waharibifu.

Mzee Boru Ali : Taalen haarraka kheesaa baana waan ann feed, oonneen tiyy, gaan dhiidhaamii saaggali khaa aarmma dhuubbaatan mooniin tiyy waan aann qaabb, issii issillaan issaan keenyaa kheessaa maan qaabba taan irraa dhuubbi qaabb jeed. Issiilaani keenya maan qaabb, moonin tiyy issiilaani keenyaa, issilaan issaan keenyaa sikaal kheessa maan qaabbnaa, aan waan siirkal kheesaa qaabb

Translator : Yeye mzee anasema, mpaka leo anashangaa mwaka thelathini-na-tisa, anauliza kweli, sisi Waislamu tuna haki gani, hapa?

Mama Jamila Bishar : Kwa hivyo tunaomba Katiba mpya aangalie haki ya wakina mama vizuri na watoto wasichana wote wasome vizuri na masomo ya bure wapatiie wasichana ili wasichana wetu washikane na Wakenya wengine. Hiyo miaka ishirini watu tuliomba hiyo masomo ya bure hasa kwa wasichana wapatiwe free, Katiba ipitishe hivi hasa wasichana zaidi zaidi. Asanteni sana.

Com. Lethome : Haya Asante mama. Mama Salo Abdi? Salto Abdi haraka haraka tumalize na Kina mama

halafu tuingie kwa kina baba tena. Salo afuatwe na Mumina Halkano.

Mama Salo Abdi : Ma-Commissioners akina mama na akina baba hamjambo?

Com. Lethome : Hatujambo.

Mama Salo Abdi : Sina mengi ya kuongea ni machache tu kuhusu akina mama.

Ya kwanza, akina mama kwa kimila yetu ya Kiborana kwa kusema Mama ‘Behind every man’s success there is a woman and behind a man’s failure there is a woman’. Kwa hivyo mwenye kusema mama arudi nyuma ameongea mbaya sana. Kwa hivyo mama awe mstari wa kwanza. ...[ululations]...

Ya pili naongea juu ya ‘girl child education’. Girl child education kwa kusema kweli sisi kwa kimila yetu Waborana, girl child education msichana akipita vizuri na mvulana akipita vizuri yule wanachukuwa kwanza ni kijana. Kwa hivyo msichana achukuliwe mbele kwa sababu wanasema msichana amezaliwa kwa sababu ya mwanaume. Sio lazima amezaliwa kwa sababu ya mwanamme kwa hivyo kwa Katiba mpya ipitishe ya kwamba msichana achukuliwe mbele. ...[ululations]...

Ya pili kile naongea ni kuhusu shule ya malazi: Shule ya malazi kwa hakika nikizungumzia wengi wao wameenda course na waka maliza ni akina mama. Sijui ni kwa sababu akina mama ndio wame hitimu hiyo course ndio wanatukalisha nyuma kwa hivyo tunataka constitution mpya ile inawekwa hata shule ya malazi ichukuliwe kama Teachers Service waajiri shule ya malazi pia.

Halafu ya tatu kile naongea juu ni cultural: Zamani culture ya Borana ni, tukona nyimbo ya culture ya Borana tuko na vitu culture ya Borana tuko na kila kitu. Kwa sasa ukienda huko Samburu ile culture yao wanaihitimu wanaiweka katika Katiba lakini yetu ya kimila yetu ya Kiborana inarudi nyuma kwa sababu tunataka culture yetu ya Kiborana iwekwe maanani. ...[ululations]... Pia sisi tuhifadhi katika Katiba mpya.

Ya tatu ile naongea juu ni kuhusu Chief ama Councillor: Hata akina mama wako na right ya kusimama councillor hakuna kusema yeze ni mama arudishwe nyuma. ...[ululations]...

Kingine naongea juu ni mama na akina Councillors, mjumbe wote wamechaguliwa na raia kama Mjumbe na Councillor. Kwa sasa Mjumbe anapata mshahara, Councillor anapate mshahara lakini akina mama hawapati chochote. Kwa hivyo kwa katika Katiba mpya tuangaliliwe masilahi ya akina mama pia hata hao wamechaguliwa na raia. ...[ululations]... Kwa hivyo kwa Katiba mpya tuwekewe na tuhakikishiwe.

Kingine ni kuhusu girl child education: Girl child education kwa... samahani nimeirudia lakini nairudia kidogo. Kuna mzee asubuhi alikuwa ameongea juu ya wanawake hapa sana anasema wanawake hawana haki, ama kimila yao wanasema ati mila ya Kiborana...

Com. Lethome : Tafadhal fanya hivi Salo wewe toa mapendekezo yako wachana na mzee alitoa yake wewe toa yako sasa.

Mama Salo Abdi : Kwa hivyo huyo mzee sasa alisema wanawake wakuwe mstari wa nyuma. Sasa sisi akina mama tumekataa, tuwekwe mstari wa kwanza kwa kila kitu. Kwa hivyo ni hayo asanteni.

Com. Lethome : Haya asante sana. Kuna huyu mama wa mwisho Maumina Halkano ama hayuko. Haya njoo Halkano. Wewe toa maoni yako wachana na mzee alisema. Wewe toa yako sasa. Mzee alisema yake wewe toa yako sasa.

Mama Mumina Halkano : Asalaam Aleykum!

Com. Lethome : Jina.

Mama Mumina Halkano : Kwa jina mimi naitwa Mumina niko na mapendekezo machache lakini...

Com. Lethome : Karibia mic.

Mama Mumina Halkano : Ngoja ngoja nitajaribu ku. ...[inaudible]... Kwa sasa niko na mapendekezo mingi. Ama ni shike.

Com. Lethome : Abdilahi njoo usaidie mic bwana!

Mama Mumina Halkano : Sasa niko na mapendekezo chache nitaongea juu lakini nime andika kwa kingereza nitakuwa nikisoma.

Com. Lethome : ... mic it is not my work...

Mama Mumina Halkano : Nitakuwa nikisoma halafu nitarudia kwa kiswahili juu.

Ya kwanza ni affirmative action: Affirmative action the principal of affirmative action should be put in place and maintained in the entire Constitution to ensure the elimination of all areas of discrimination and facilitate the equity and justice for all. Hii tunaongea juu ya usawa tunasema, hatusemi kimaumbile tuko sawa na wanaume lakini tunataka usawa. Mama watoto na wale hawajiwezi lazima wapatiwe haki yao sawa na wanaume wote. Na tunataka kwa muda hii affirmative action tunataka usawa hio itiliwe kwa Constitution ipitishwe affirmative action ikuwe itafanya akina mama na akina baba wakuwe na nafasi sawa kwa employment ama kwa education.

Ya pili ni constitution: The Constitution should provide a guarantee of equal access by men and women to all resources including land. Wanaume na wanawake wakuwe na equal access ya land ardhi na property. Wakuwe na equal access, usawa hata hio tukuwa na usawa kwa mali kwa ardhi kama ni title deed mwanamke akuwe na haki ya kupata hio.

Pendekezo la tatu. The new Constitution order should provide for a social security scheme for persons with disabilities particularly women in terms of basic needs eg. Housing, clothing, health and food. Hii Constitution sasa tunataka Constitution mpya tuwekewe kwa wale wasiojiweza wapate basic rights kama manyumba, kama chakula wapate free yote.

Pendekezo langu la nne. The Constitution should create a Ministry for gender and women affairs with a specific department dealing with disabled women and girls. Wale wamama wasiojiweza wale mavu wapatiwe nafasi ya kwanza kama nomination ya Mp wakuwe nominated instead of wale wanajiweza wana-appoint-iwa wanakuwa nominated. ...[ululations]...

Pendekezo langu la tano. Kadhi's court should be made into a separate set of courts with appeal to an Islamic division of High Court. Hii sasa wengi wameongea juu ya hii Kadhi's. Tunataka hii Kadhi's court ikuwe na court of appeal. In case tukishindwa na hii kesi tuweze ku-appeal above. Tunataka Kadhi's Court of Appeal ikuwe kwa hii new Constitution.

Ya sita ni appointment of Kadhi's should not be by Judicial Service Commission but should be by Ullumaa Tunataka asi-appoint-iwe na Judicial tunataka Ullumaa achaguliwe na Kadhi.

Ya saba Muslim women who are working in the Civil Service when their husband dies, their mourning period of four months and 10 days should be given leave all this period with full payment of their salaries. Wakina mama wakiwa Bwana zao wanafiwa lazima wapate hiyo nafasi ya mwezi nne na siku kumi halafu wakae wakiomboleza ya kwamba bwana yao amekufa wapate nafasi, wapate mshahara wao wasikatizwe kazi zao. ...[ululations]... Tunaomba hiyo ipitishwe kwa sheria mpya.

The victims of 1967 Shifta wars should be compensated through affirmative action. Wengi wameongea juu ya hii ya 1967 shifta war. Tunataka sasa hii Katiba ipitishe ya kwamba tukuwe compensated tulipwe tupate usawa na wale wanakaa down country na hawa watu wa Northern Frontier tulipwe haki zetu ile damu tulimwaga hii poverty yetu imetokana na hiyo tunataka tulipwe tupate usawa na wale wanakaa down country usawa kama ni mali yetu, mifugo yetu yote ikuwe tunalipiwa. Tukuwe na sawa na hawa tupate kila kitu.

Ya nane yangu nikisoma. Equal distribution of natural resources: Hii sasa tunataka kama natural resources, wengi wameongea juu kama hii ya nini yote. Tunataka tukuwe na equal distribution akina mama na akina baba wote sawa wapate hiyo tuandikiwe kwa Katiba ipitishwe ya kwamba tutakuwa na usawa ya hiyo pia tupate. Hata kama ni Serikali na raia wapate equal distribution vile wengine walikuwa wamesema hapa awali.

The Kenyan Constitution should provide that all citizens are equally entitled to rights and privileges and benefits of citizenship regardless of gender. Hii sasa ningesema juu ya citizenship if today a man will marry a foreigner that woman will become a Kenyan citizen. If a woman marries a foreigner the man will not become a citizen. Tunataka ipitishwe ya kwamba it should be both sides.

Com. Lethome : What you do Mumina don't elaborate your points just make your recommendation so that you cover everything.

Mama Mumina Halkano : Okay. The Kenyan woman should suffer no form of discrimination operation that reduces her dignity and extreme as a Kenyan. Mwanamke apatiwe... wacha unajua hawa fahamu wengine.

Com. Lethome : Okay

Mama Mumina Halkano : Ndio napenda at least ni yapitie

Com. Lethome : But although it is meant for us but go ahead.

Mama Mumina Halkano : It is meant but they want it I know. Lazima wanawake na watoto wasi-discriminate-iwe yaani wasi patiwe nafasi yao isisemekane huyu ni mama hawezi kuwa kwa hii nafasi huyu nini, lazima mama na baba waangaliwe kwa usawa wapate nafasi kama ni kazi waajiriwe wapate nafasi sawa.

Kwa upande ya watoto. No child shall be separated from her mother before attaining the age of 18 but all the basic necessities should be provided for by the father. Watoto mama na baba wakiwachana watoto lazima wakae

na mama kwa muda wa miaka kumi-na-nane mpaka wahitimu hiyo miaka wakae na mama lakini baba awe akiwapatia malezi.

Na tena kuna moja ingine imebaki. Any child separated from the father shall have the right to maintain personal relations or direct contact to the father. Ni sawa kwa upande ya baba pia mama akichukuwa watoto lazima awe na uhusiano mzuri na mama na lazima angalie watoto wakiwa wamekaa mahali tofauti.

Sasa nitakuwa nikisema zangu. Kuna hii Serikali tulikuwa nasema watu wengi walikuwa wameongea wanasesma wanataka Majimbo. Hii majimbo ni kweli tunataka hii majimbo lakini tunataka kama mjumbe mheshimiwa amesema Nfd. Majimbo ya upande huu wetu. Tukisema labda ya nini Borana haiwezi kuwa. Tunataka hio ikuwe Nfd na ikuwe at least tukuwe na pastrolists wakuwe na haki yao tuwe tuna value kile kitu –what we have- so tunataka Serikali ya majimbo.

Na ninaomba Constitution ipitishe terms. The President should be above the law. His terms should be two terms that is ten years and the same as the Parliamentarian the same as Civics. Wajumbe na ma-councillors wote lazima wakae two terms. Isipite two terms. Ikipita two terms hiyo imekuwa too much. Isipite two terms wakae two terms na two terms hiyo nimewapatia mingi ni ten years. Kwa hivyo mtu akikaa ten years kama amefanya maendeleo ama hajafanya ata kaa. Lazima akae naipitishwe pamoja ya Rais. Ninaomba hiyo.

Na tena siwezi kutaja mtu lakini kuna wenzetu wamesema wamama hawana haki ya kwamba they are not, hawangefaa kupigania kiti cha President. Wamama wako na haki usawa na wababa lazima wasimame wakitaka leo hii wakijiskia wasimame u-president ama nini lazima wasimame. Wasimame waombe raia, vile wengine waliomba waombe raia wasimame. Kwa hivyo wamama na wababa nisawa lazima hata wakiomba hakuna kusema ati hana aibu kusimama. Hakuna aibu yoyote yeye atakuwa naye lazima asimame na ni wote wataomba raia.

Tunaomba hii discrimination ya kusema mtu akikufa mtu akiuwa mwanamme akikufa apate 100 animals na mwanamke ni 50 it should be equal. Ni lazima iwe sawa nafsi ni moja it should be equal, lazima tupate nafasi sawa. Asanteni kwa hayo.

Com. Lethome : Asante. Pengine ningeonya tu kitu kimoja nafikiri kama Muislamu kuna jambo ambalo siwezi kunyamaza ikisemwa hapa. Tafadhalini Kina mama mnapozungumzia juu ya haki za akina mama msivuke mipaka ya dini. Itakuwa tumekasirisha Mwenyezi Mungu Suna Allah Wataallan. Mnataka kumkasirisha mwenyezi Mungu. Basi kwa hivyo tuseme wanawake wapewe haki kulingana na sheria ya mwenyezi Mungu. Ama sivyo? Wasinyimwe haki zao lakini tusipite kitabu cha mwenyezi Mungu. Ama sivyo? Sawa. Haya tumpate Hassan... ni Hassan Godama ama Golma. Galma Yuko? Ashazungumza. Hussein Galgalo Jahani? Rapsuban? Hussein

Mandera? Huyu alizungumza jana kule. Mandera? Hussein Mandera alizungumza jana Modogashen Hussein Mandera yuko hapa? Huyu hakuzungumza.

Mr. Hussein Mandera : Kwa bahati njema nimepata nafasi hata sijui vile nime itwa hapa. Mimi nimesema kwamba tangu...

Com. Lethome : Anza na jina!

Mr. Hussein Mandera : Jina langu ni Hussein Mandera kutoka Garbatula. Since independence ile maendeleo Serikali inatupatia ni mambo ya relief food na kama hii relief food inarudishwa kwa pesa ni pesa mungi sana. Mimi napendekeza ya kwamba kwa hii Katiba iwekwe ya kwamba hii pesa ya relief food iwe kitu kama revolving fund tuanze biashara tofauti tofauti. Kwa sababu mkiona hii pesa ya relief, relief huletwa kutoka Mombasa mpaka Garbatula hiyo ni pesa nydingi sana.

Ya pili we have potential natural resources kitu kama gum arabic, minerals, just to mention a few therefore the Constitution through the Ministry of Natural Resources should allocate some budget, tuwekewe budget ya kwamba hata sisi tupate access kwa soko, I mean kupata soko ya hizi vitu ili tupate mapato. Pia hapa Isiolo wilaya hii yetu ya Isiolo head of departments, wale wanaongoza departments zote ni watu kutoka southerners. Bado sisi tungali katika ukoloni wa waafrika. Hawa ni locals. Wale hawana haja, they don't have sense of ownership for anything that comes to our District. Therefore hata sisi pia tuko na wasomi. Sasa mimi naona katika Katiba ifanywe kwamba at least wasomi wetu pia wawe head of departments ili District yetu ya Isiolo iendelee mbele. Asante.

Com. Lethome : Watu wote wangefanya kama Hussein tungemaliza kabla ya magharib. Huka A Kolumbola? Ameongea – Alhamdulilahi! Hassan Guyo amezungumza pia! Abdulahi Kulicha? Ameshazungumza huyu. Osman Dima? Adan Abdi? Ali Guyo Abdi? Roba Dabaso? Guyo Koto? Jaro Forole? Huyu ni nani? Haya Osman endelea. Tutafikia kila mtu Inshallah! Sema jina halafu zungumza.

Mr. Osman Dima : Jina ni Osman Dima.

Com. Lethome : Endelea

Mr. Osman Dima : Ningenegea Kiborana lakini muda unaonekana ni kidogo wacha mimi na tumia tu Kiswahili.

Com. Lethome : Tupa tupa tu!

Mr. Osman Dima : Maoni yangu ni mawili, matatu tu sababu hata nafasi ni kidogo. Maoni ya kwanza jina ya District hii wanasema Isiolo District irudishwe kuwa Borana District. Badala unasema Isiolo District useme Borana District.

Com. Lethome : Haya ingine.

Mr. Osman Dima : Maoni ya pili sheria ya Borana vile wanafanya court ndio wanafanya nyumbani. Na wanasaidia watu sana. Kwa hivyo sheria leo iingize hiyo sheria ya Borana iwe halali sababu zamani inaonekana kama wamebakisha nyuma.

Ya tatu naongea kidogo juu ya mifugo. Sisi hatuna shamba kitu tukonaye kwa ardhi hii ni mifugo. Mifugo wakati sisi tunauza moja mbili lazima tunalipa pesa. Tukitembea barabara kama sisi napeleka na gari tukilete soko kuna pesa tunalipa. Lakini wakati Jilali wanamaliza hii maliza hii mali hakuna pesa yoyote wanaletea sisi. Tunataka sheria ya leo ingizwe malizwa na Jilali ama na ugonjwa Serikali ilipe.

Com. Lethome : Jilali ni nini?

Mr. Osman Dima : Jilali ni Ukame. Kiswahili kidogo kidogo tutajifunza. Ya nne maoni yangu nitasema juu ya wanyama wa pori. Wanyama wa pori ni wetu si wa Serikali. Sijui saa zingine tunashangaa sana kusema wanyama wa pori ni wa Serikali. Mnyama wa pori Serikali wamenunua kutoka wapi? Ilikuta hapa. Na sisi pia tume kuta mnyama wa pori hapa. Tunataka Serikali iwachie sisi hawa wanyama sababu wametudhulumu. Wanyama wa pori ni wetu. Sisi ndio tutafuga. Sisi ndio tutauza. Tunataka iingizwe kwa sheria wanyama wa pori wawe wote wa wananchi. Kwanza Serikali imetudhulumu mnyama wa pori amewekwa kwa kijiji na amefanywa adui wetu. Mnyama wa pori wa kawaida ako humu humu hata hakuli ng'ombe wanakula moja moja. Hata ndovu ya humu humu hakuna wakati wanaumiza mtu. Lakini hayo mnyama ana umiza mtu huyo wananchi wanalamika ni ile imewekwa kwa kijiji wanafanya adui yetu. Vile tumefanya huyo mnyama hata tukifanya mnyama huyu wetu wa kawaida wa boma. Ikitengwa na sisi watakuwa tu namna hiyo adui. Kwa hivyo mimi maoni yangu nataka mnyama wa pori Serikali irudishie sisi sababu wanadanganya sisi na wanadhulumu sisi.

Com. Lethome : Asante

Mr. Osman Didi : Yangu ni hayo machache.

Com. Lethome : Asante. Sasa mwenye ku-record pale analalamika anashindwa ku-record. Ile tape recorder yake ikifika Nairobi itakuwa na kelele nyingi sana. Kwa hivyo mkishangilia kidogo mnampatia nafasi wakati mtu anazungumza ndio aweze ku-record. This is historical, you know, this is something historical. Hii kitu itawekwa Kenya mzima watajua watu wa Garbatula walisema kitu gani. Five hundred years to come. Wajukuu na wajukuu watakuwa wakisikiza hiyo cassette. Huyo kijana atakuwa ni babu siku hiyo. Wewe uta kuwa ni ayeyo siku hizo. Inatakiwa hiyo record iwe clear. Kwa hivyo tafadhalini tupunguze kelele. Haya tusikize Mohammed Tuka kama yuko? Tuka yuko? Hayuko? Mohammed Ali Jare? Hayuko? Idris Boru Ali. Haya. Halafu Adhan Dege afuate.

Mr. Idris Boru Ali : Asala Mualeykum Aleykum! Waramatulah Wabarakatu. Kwa majina mimi naitwa Idris Boru Ali kutoka Kinna.

Mimi pendekazo langu ya kwanza nina anzia na Arms of Government. Arms of Government. There are three arms of Government Judiciary, Legislature and Executive. Katika hii sheria ambayo tuna unda sasa ningependa kusema ya kwamba let these three exist but all of it to be independent bodies, Judiciary to be independent, Executive to be independent, Legislature to be independent.

Ya pili kuhusu hiyo under the Judiciary Kadhi anafaa kuwa na uwezo sawa na mahakimu wa Serikali. He should have equal powers with Government Judges. Ya pili makadhi wanafaa kuteuliwa na Maglisual Ulamaa board of ...[inaudible]... Kwa sababu ...[inaudible]... ndio wanafahamu dini sawasawa na wao ndio pia wanafahamu masharti ambayo Kadhi angefaa kutimiza. Sio Presidential appointee wala Public Service Appointee. Makadhi wachaguliwe na body.

Inginge pendekazo langu kati miji ya Waislamu bars za pombe hatutaki kwa sababu dini yetu haikubali na hata mila yetu haikubali. Hata dini ya Kristo haikubali. Mimi pendekazo langu kuhusu hii pombe ipigwe marufuku. Beer to be illegalized to be banned in this Constitution that we are forming now.

Pendekazo langu lingine, katika court ya Serikali tunataka sheria mpya iwekwe ya kwamba Muislamu asiiname akiingia court. Pendekazo langu lingine, tunataka sheria mpya iwekwe ya kwamba Judge Mkristo au mtu Mkristo asishike kitabu tukufu ya Koran kwa mkono wake.

Pendekazo langu lingine, Ijumaa iwe siku ya mapumziko ya Waislamu kwa sababu ya sala ya Ijumaa ambayo ni muhimu sana. Pia ningependa kusema mwezi tukufu wa Haj Waislamu ambayo wako na uwezo ya kuenda siku hiyo wasiweze kuenda siku hiyo kwa sababu ya ukosefu ya nafasi wala si ya mali. Hii haswa ni kwa wale ndugu Waislamu ambaye wana fanya kasi ya Serikali.

Com. Lethome : Unapendekeza nini?

Mr. Idris Boru Ali : Ninapendekeza wakati ya Hija wapewe ruhusa wakiwa na uwezo huyo. Please. Pendekazo langu lingine katika sheria hii ambayo tunaiunda sasa. Ningependa kusema wanaume na wanawake wasikuwe sawa. Kwa sababu hata tukiunda sheria simzuri kupita kitabu tukufu cha Mwenyezi Mungu. Kwa sababu mwenyezi Mungu amesema ...[Arabic Dialect]... mwenye atavuka mpaka ya mwenyezi Mungu amedhulumu nafsi yake. So kwa hivyo ningepende kusema wanaume na wanawake wasikuwe sawa.

Pendekazo langu lingine Waislamu wakifa hospitalini wasipelekwe mortuary. Waislamu wakifa hospitalini wasipelekwe mortuary ili wazikwe haraka.

Ningependa kusema tena family planning kwa sehemu ambayo Waislamu wanaishi isiletwe kwa sababu dini yetu haikubali family planning. Madawa hizo haziletwi kwa ile sehemu Waislamu wanaishi. Pendekazo langu lingine, la mwisho ningependa kusema Chief Kadhi awe na equal power na Attorney General na awe na haki ya kuingia katika Parliament.

Com. Lethome : Asante ndugu.

Mr. Idris Boru Ali : Pendekazo langu lingine wasichana wakubaliwe kuolewa hata wakiwa masomoni. Kwa sababu dini yetu haikatai.

Com. Lethome : Maoni yake wacha amalize. Sheikh umemaliza? Haya asante ndugu yangu kama umemaliza maoni yako.

Mr. Idris Boru Ali : Sijamaliza!

Com. Lethome : Naona unapewa maoni sasa mengine hapa.

Mr. Idris Boru Ali : Sipewi.

Com. Lethome : Basi ya mwisho sasa tafadhali.

Mr. Idris Boru Ali : Maoni yangu ya mwisho ningepende kusema wasichana hata wakiwa shulenii hata wakiwa masomoni wapatiwe ruhusa ya kuolewa.

Com. Lethome : Hiyo umesha sema. Unarudia. Basi kwisha.

Mr. Idris Boru Ali : Ningependa kusema ya mwisho, katika hii sheria ambayo tunaunda sasa waalimu, teachers, should be favoured amongst the other civil servants. Mishahara yao iangaliwe vizuri.

Com. Lethome : Okay. Are you a teacher?

Mr. Idris Boru Ali : I am not.

Com. Lethome : Okay. Adhan Dege? Halafu afuatwe na Abduba Mollu Idu? Yuko? Mollu? Haya!

Dr. Adhan Dege Guracha : Commissioners walioko, viongozi na wakaazi wenzangu, Asalaam Aleykum! Na shukuru mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii na ingawa naambiwa masaa ni mabaya. Hata hivyo kabla sijafika kwa recommendations zangu, kwa sababu yangu itakuwa ni moja moja. Recommendation 1, 2, 3 lakini kabla ya hapo nataka kwa manufaa ya wale Commissioners walioko hapa kutanguliza kitu kidogo ili wafahamu vile hali ilivyo katika area hii yetu ya pastrol area. Watu wote wa hapa huwa wanassema mtu akitoka Nairobi au akienda Nairobi kutoka Isiolo anasema yeye anenda Kenya. I want this to be understood in this perception, in this light, kwa sababu ya sisi kusema tunaenda Kenya au tumetoka Kenya ni kwa sababu hali tunayoishi hapa haionekani ni kama ya Kenya. Tuko nyuma, tume nyimwae kila kitu, tumedhulumiwa ndio sababu sisi tunassema tunaenda Kenya, as if we are not in Kenya, that is the actual meaning of the community of this area. I want it to be understood in this light.

Na tafadhali, samahani, tafadhali tafadhali usipige makofii. Nataka isikike wenye ku-record wa record vizuri kwa sababu ni kutoa maoni. Kwa hivyo mimi ningependa kusema ya kwamba yale mambo yanatendeka hapa sio ati yote haiko katika Katiba ya Kenya la! Mambo mengi yalikuweko. Yale mambo yametajwa na watu hapa awali ni mambo yalikuwa katika Katiba kuanzia mwaka wa sitini-na-tatu. Lakini kilichoko ni ya kwamba wale walikuwa katika Serikali hawakutia maanani, hawakuifuata.

Wangeliifuata saa hii sisi hatungekuwa na umaskini. Kwa sababu walisema in 1963 one of the policy papers ilikuwa inasema kutafanywa a comprehensive livestock development and marketing package in arid and semi-arid areas. Kama ingefanyika sisi wengi wetu wote hapa hatungehitaji msaada wa Serikali. Kwa hivyo maombi yetu ya leo ni kusema baadhi ya yale mambo yalisemwa mwaka wa sitini-na tatu, kama ilikosa kufanyika tunaomba sasa ifanyike. Na baadhi ya haya mambo ni kama yafuatayo.

Kugusia juu ya livestock. This is the communities economic mainstay. This is our lifestyle. Ni kama Wameru

wako na shamba. Ni kama huko upande ya Kericho watu wako na shamba ya mahindi. This is our lifeline. Kwa hivyo tunataka improvement on this lifeline. Recommendation yangu kuhusu improvement ni ya kwamba Board ya Livestock Development and Marketing iwe established like any other product kama majani na kahawa. Let this economic mainstay be recognized like any other product in this country. Unajua kuwa Mkenya sio jina, ninaamini hatakuwa Muislamu sio jina ni kuwa katika mwenendo ya Muislamu. Sisi hapa tunasema we are in Kenya but we don't live like Kenyans. All we want today is to live like Kenyans.

Na ya pili katika kuhusu mambo ya livestock wenyeji wahuishwe na soko itengenezwe. Soko ambapo itapoteza au itazuwia gharama ya kutoka Garbatula kwenda Nairobi kupeleka mifugo. Kama kuna soko hapa, for example hapa kulikuwa na soko hapa Garbatula zamani na wengi wa viongozi wetu walisoma kutokana hiyo soko kwa sababu kulikuwa na ushuru ya kuwalipia fees na kujenga shule wakati huo. This is pre-colonial.

Na ya tatu ningependekeza ya kwamba kichinjio, abattoir, iwe set-up strategically in this pastoral area. Kwa mfano kuna mahali hapa kulikuwa na kichinjio hapa about 10 to 12 kilometres from here. Ilikuwa inaitwa Korogocho. Wakati wa ukoloni. Mahali ng'amia ilikuwa inachinjwa inakuwa packed, na ili kuwa inauzwa. Wenyeji walikuwa wananaufaika na hakukuwa na hasara hata wakati wa ukame ukiuza ng'amia yako hapa unafaidika, it is about 12 kilometres from Garbatula town. Kama kitu kama hicho kina weza kufanyika ingekuwa vizuri.

Na ya nne ningependa kupendekeza ya kwamba appropriate range land management policies iwe in place. Hata kama ilikuweko kwa Katiba haikuwa imefuatwa. We were not consulted. Sisi wenyeji hatukuhuishwa kile kinafanya ni kutoka Nairobi, watu wanaamua kutoka huko inakuja hapa Isiolo I mean au Garbatula. Kwa hivyo there was lack of ownership.

Kuhusu ardhi, nafikiri mambo mengi yamesemwa, sita sema mengi, lakini mambo ya Trust Land iwe abolished. An appropriate system of land tenure iwasilishwe ikiwa imewahuishwa wenyeji.

Na ya pili kwa upande wa ardhi. Those settlement areas for example like Garbatula, Isiolo these are urban centres, if possible land iwe demarcated iwe Title deeds ziwe issued so that watu waweze kupata title deeds. Haki ya kumiliki ardhi. Kwa sababu kama huna haki ya kumiliki that means sisi si watu wa mifugo kwa sababu mifugo inategemea ardhi hii. Kama hii ardhi ikienda hata mifugo haina kazi.

Kuhusu establishment of game parks au reserves yangu ni mawili tu. Moja wenyeji wa area hiyo wahuishwe wawe consulted, not partial consultation. Wahuishwe wakae chini wazungumze wakubali. Na mahali ambapo imekubaliwa, in cases where establishment of game reserves or parks is agreed upon the residents should benefit directly and substantially. This is my recommendation. Be it in form of compensation, be it in form of

development projects.

Com. Lethome : 1 minute Daktari.

Dr. Adhan Dege Guracha : Okay. Kuhusu chiefs. Ikiwezekana Provincial Administration iwe abolished. Lakini kama haitakuwa abolished chief awe not below form four D⁺. This is my recommendation. Kuhusu Government ministries ningependekeza ya kwamba ministries ziwe de-centralized, if we de-centralize this economic distribution will also come in. Kuhusu mtindo wa kiserikali mimi recommendation yangu ni kuwe na Regional Government. Nafikiri mengi yamesemwa juu ya Regional Government.

Kuhusu mambo ya Id's Birth Certificates and Passports. My recommendation is Id cards iwe issued continuously. Birth Certificates iwe issued at district and divisional levels. Passports iwe issued at district level. I am one of the victims I had to run after a passport for eleven months with all costs.

Kuhusu inheritance my recommendation is the Islamic system of inheritance be enshrined in the Constitution. Hatungelipenda mambo iwe kama 1980 wakati ambapo hoja ilipitishwa Katiba bunge sisi turithi vile Wakristo wanarithi wenzao. Islamic education should be taught in all schools upto University level that is my recommendation.

Education for all children should be made mandatory. Free education should be enshrined in this Constitution.

Hapa nitawaunga kina mama mkono. Kuhusu wasichana wale wanatolewa kwa shule wakaolewa. Mimi ninge-recommend hiyo ihalalishwe. Na kama mtu amepatikana ametoa msichana wa shule na akaiza mtu, stiff penalties be enshrined in this current Constitution. Pia kwa yule baba na kwa yule mtu anataka kuoa.

Kuhusu Kadhi's Court. Mimi na-recommend hivi. Kuwe na District Kadhi's Court, Kadhi's High Court na kuwe na Kadhi's Court of Appeal. Kwa sababu ukifika Court of Appeal yule Judge atakuwa yule atakayesikiza kesi yako pengine ni mtu sio Muislamu, kwa hivyo hana fahamu ya sheria ya Kiislamu, kwa hivyo ni vizuri tuhukumiwe kwa sheria ya Kiislamu.

There is one very contagious issue. Kuna barrier moja hapa Isiolo. Hii ilikuwa ni mtindo wa Serikali ya ukoloni kutufungia tusiwasiliane na maendeleo kwa areas zingine. My recommendation is hiyo barrier ya Isiolo is the only one which I believe exists in Kenya apart from the boarders. It is as if we are on the boarder. I have been to Namanga and I have seen a barrier, I have been to Busia I have seen a barrier, I have been to Mandera I have seen a barrier, I have been to Moyale, but it is similar to the one in Isiolo. Hiyo ni mtindo ya kutufungia sisi. It is to

create fear watu waogope kuingia kwetu. Na watu wakiogopa kuingia hakuta kuwa na maendeleo. For the same system.

Com. Lethome : Asante. Tafadhali maliza.

Dr. Adhan Dege Guracha : Nafikiri kwa sababu mengi yamezungumzwa na muda pia hapa ni haba. Yangu ni hayo tu. Na nasema shukran.

Com. Lethome : Asante Yusuf Dogo? Yuko? Abduba? Gtdo ye ye ana maandishi halafu afuatwe na Yusuf Dogo kama yuko. Yusuf Dogo?

Mr. Abduba Mollu Idu : Asalaam Aleykum! Mimi sita ya rudia yale yamesemwa. Lakini nitagusia tu yale ambayo nafikiria hayajaguswa na wenzangu wale wameongea. Ya kwanza ningetaka kugusia aina ya Katiba. Tungeuliza Katiba ambayo tunatengeneza sasa ikuwe, iandikwe katika lugha ya Kiswahili na pia kwa lugha ya kingereza. Na pia ikuwe inaweza kupatikana kila mahali, public places, kwa mashule, na libraries free of charge. Na pia wale wanataka kununua ziwekwe, hii Constitution ikuwe kila mahali in bookshops so that kila mtu anaweza kusoma na kuelewa ni sheria gani ndio inamuongoza.

La pili nasema hii Katiba pia iandikwe kwa lugha rahisi ikuwe clear na pia iweze kufuutiliwa. Kuna swali ambalo tunajiuliza katika siku za usoni. Hii Katiba ya mbeleni inaonekana haijakuwa enforced? Hii Katiba ingine lazima ikuwe enforceable na pia maongozi haya ambayo yatakuwa katika Katiba yawezekuwe kufikia kila mtu kwa njia ya Civic Education. Tunaamanisha ya kwamba Civic Education iweze kuweko even after Constitution imetengenezwa. Ili watu wawezekuwe kuelewa ni nini ina waongoza. Nimesema sita ongea kila kitu kwa sababu tumeandika.

Jambo lingine ni kwamba tumesema Provincial Administration ifutiliwe mbali. Hiyo haina maana kwetu na tunaona badala yake Local Authorities ikuwe empowered na wakuwe sensitive to the needs and aspirations of all citizens.

Tuingie mambo ya Legislature najua haya hayajaguswa kabisa tunaongea mambo ya wajumbe. Tumesema ya kwamba kuwa mjumbe awe na full time job. Nina maana gani? Wajumbe wana mshahara kubwa lakini unakuta ya kwamba wajumbe wako at their own discretion wanaingia Bungeni mtu anakaa three minutes, five minutes ame register for his allowance ametoka. Maswali yanakuja mjumbe hayuko, Minister hayuko. Kwa sababu anakula mshahara kubwa kubwa tunasema kazi ya mjumbe ikuwe full time job, since they are paid fully. Na pia tunasema mjumbe akuwe na ofisi katika mahali ya uwakilishi Bungeni. Na pia akuwe na wafanyakazi ambayo wata hudumia raia katika hizo constituencies. Sio Mjumbe atafutwe in the streets of Nairobi.

Pia tunasema ya kwamba wananchi ama raia wale wanachagua mjumbe wanahitaji protection. Wanahitaji protection kutoka kwa mjumbe wao. Kwa sababu mjumbe anasema nita watengenezea barabara, nitawatengenezea hospitali, tuwe na sheria ya kwamba mjumbe ambaye hatatimiza yale amesema atafanya, badala ya kupeana lip service wakuwe na system ya ku-complain to the Parliamentary Service Commission through the Speaker of the National Assembly for summoning and eventual redress. Watu waki-complain mjumbe aweze kugolewa hata kwa siku tano.

Pia tunasema kazi ya Parliament ikuwe na Calendar of activities yake ambayo inajulikana na raia wote isiwe tu President aweke ama a-dissolve Parliament wakati anataka, ikuwe na programme yake na shughuli zote za Serikali zikuwe na programme ambayo zinaweza kujulikana.

Tumesema pia Presidential Election ifanywe kando na elections zingine kwa sababu Presidential Election is a National issue and should be treated on its own. Tunasema ya kwamba kura ya President ikuwe kando na kura za wajumbe na councillors. Kwa sababu hapa area hii yetu kuna hiyo tunaita mlolongo ama-line. Nikipigia president wa Kanu, lazima ni pigie mjumbe wa Kanu, lazima ni pigie councillor wa Kanu hiyo inafanya raia wasi-choose viongozi wazuri. So tunasema presidential elections ikuwe kando.

Na pia defections. Kuhama chama. Tunasema hiyo ifutiliwe mbali kwa sababu hiyo inaleta shida. Kama umeshindwa kwa Kanu kaa mbali. Kama umeshindwa kwa Dp ukae mbali usirudi na chama kingine.

Pia tunasema kwa sababu president is a national office the occupant of this position should not be an elected Mp. Yaani asikuwe na uwakilishi bungeni. The constituency of the president is the whole country asikuwe mjumbe wa baringo central.

Com Asman : Maliza maliza tafadhalii.

Mr. Abduba Mollu Idu : Hapa pia tunaulizwa kuhusu mambo ya Public Service. Yaani Watumishi wa Umma na tumegusia hapa mambo ya utumishi wa umma. Tunasema ili Kenya ikuwe na watumishi wazuri ambayo wanaweza kufanya kazi vizuri tunesema kwamba the state should ensure that there is proper working environment for all public servants. There should be proper recruitment and placement based on competence, qualification and experience.

Tunamaanisha kwamba watu wasiajiriwe kazi kwa sababu wako na mtu fulani katika cheo kikubwa. Watafute wale ambayo wako na kipawa cha hiyo kazi, wako na-competence na-experience ndio ifuate badala ya kusema niko na

mjumbe wangu niko na minister fulani ndiyo nina weza kupata kazi mahali fulani. Pia tunasema wapewe nyongeza za mshahara na pia wapewe public service isikuwe na mambo ya corruption na political interference. Constitution i-protect hiyo.

Mambo ya Natural Resources imeongewa sitaongea sana. Inasemekana ya kwamba local communities mahali natural resources ziko waweze kufaidika na wahusishwe katika protection. Watu wanafikiria natural resources ni madini tu ya Duse. Hata mchanga wa hapa ni natural resources yetu. Mchanga hapa kila siku lorry kumi lorry ishirini. All natural resources hata hii miti ni natural resource. Mtu anakuja anakata, mawe zinaokotwa all these things are natural resources. So tusifikirie tu natural resource ni wildlife, yote ikuwe protected.

Nina kuja kwa participatory governance kwa sababu pia hapa haija ongelewa na watu wengine. Tunajua ya kwamba Civil Society organizations ama mashirika yasio ya Serikali yana jukumu kubwa na tunaweza kusema ya kwamba kama sio mashirika yasio ya kiserikali area nyingi ya Kenya hasa arid areas hawangeweza kufika mahali wamefika kwa sababu wamewachwa mbali na Serikali. Majority of civil society organizations especially Ngo's have worked with and amongst the people in different sphere's of life. This organizations have all along depended on external donors from the north ama Western. For how long?

Ninatoa pendekezo hapa kuhusu Civil Societies. Tunasema there should be a provision for some strategic Ngo's na Civil Societies waweze kupewa pesa na Serikali iliaweweze kuhudimia raia. Civil Societies, Ngo's wanapata msaada kutoka nje na wanasaidia raia wa Kenya, pesa zitengwe katika miradi ya Serikali na waweze kupewa pesa. The Constitution should make provision for sourcing of funds from national and multinational corporations individual citizens and consolidated fund. Ili waweze kufanya kazi yao vizuri.

Kumalizia nasema ya kwamba. Mechanisms should be in place to ensure maximum participation ya kila mtu katika Serikali na hasa governance by women, youth na persons with disabilities. They should be included in decision making at all levels. Wanawake wasiwachwe nyuma kwa sababu ya kijinsia. Hayo yamesemwa mara mingi. Wahusishwe kwanzia grass root mpaka national levels. Na pia the Constitution should recognize the disadvantaged position of these groups and lay out strategies for uplifting their position in society so that they are at par with other Kenyans. Na pia kwa hiyo class ya vulnerable groups tunataka kuuliza Commissioners waongeze pastrolists. Pastrolists are vulnerable groups. Tunataka wakuwe considered as vulnerable groups. Asante.

Com. Lethome : Asante Abduba. Yusuf Dogo? Kama hayuko karibu tunamtaka Zainab Wako? Yuko Zainab Wako? Hayuko? Somo Roba? Afuatwe na Ahmed Noor Wako? Wafuatane hivyo hivyo halafu Hussein Roba afuatwe na Hussein Abdalla Sheikh amfuate.

Mr. Somo Roba : Asalaam Aleykum! Mimi sina mengi ya kusema kwa sababu naona kila mmoja anapewa dakika mbili mbili na afadhali ni zungumze maneno kidogo kidogo ili kila mmoja apate nafasi ya kuongea. Naona hapa na pale watu wanasema mimi nimewachwa mimi nimewachwa. Kwa sababu sisi tumekuwa wengi na mwingine akishika hapa hawezi kuwacha. Kwa sababu wewe toa point yako moja moja...

Com. Lethome : Sasa toa yako

Mr. Somo Roba : Mimi naitwa Somo Roba. Sasa mimi sina mengi ya kusema maneno yangu ni haya. Maneno mimi naongea ni juu ya ...[inaudible]... Abadilishe hii mambo mtu akipatwa na makosa ashikwe maramoja apelekwe aandike statement yake apelekwe Kotini kama sheria inafunga afungwe. Lakini sio anakuja kuota hapa kwajili mtu anakaa hapa miezi miwili moja peleka Isiolo anakaa miaka tatu nne. Naona maisha yake inapotea akipelekwa remand. Kwa sababu ukisha pelekwa maramoja Kotini makosa yake ikipatikana anafungwa anamaliza kifungo chake anatoka, Kwa hivyo Serikali iweke hiyo sheria wale wanaunda Katiba iwe Katiba mwaka huu waweke ndani sheria hii ibadilishwe. Kwa sababu hii ni dhulma moja kubwa sana. Baadaye mtu hana hatia...

Com. Lethome : Mbona unarudia. Hiyo umemaliza endelea...

Mr. Somo Roba : Kwa hivyo hii mambo imalizwe kabisa iwekwe ndani ya Katiba. Maneno ya mwisho yangu ni hii. Mambo ingine mimi naongea Mr. Dege mambo ya barrier. Hii barrier naona imewekwa hapa askari wako hapa. Na ninaona mambo mingi ya magendo inapita hapa. Huwezi kuona mtu hata mmoja anashikwa anapelekwa jela. Huyu mtu anapelekwa kwa Polisi anakaa huko anakaa siku mbili tatu wanachukuwa pesa anawachwa.

Barrier sababu inawekwa ni sababu ya usalama naangalia kitu mbaya na mzuri. Sasa hii barrier lazima itolewe tuwe free gari itembee. Magari kutoka Isiolo wakitaka kupita hapa wanaogopa hii barrier. Juzi lorry ingine kutoka kule wanasema labda sisi tuko na bomb tunasema hatuwezi. Kwa sababu huko ukipita Garbatula Police watashika sisi hapo. Wanakataa.

Com. Lethome : Hii imeandikwa nyingine.

Mr. Somo Roba : Kwa hivyo hii iondolewe iwe barabara sawasawa sisi tupate uhuru tutembee. Asante sana.

Com. Lethome : Asante. Ahmed Noor Wako? Haraka haraka. Mr. Hussein Roba yuko karibu? Roba. Ameshatoa!

Mr. Ahmed Noor Wako : Asalaam Aleykum!

Com. Lethome : Badayake Hussein Abdalla.

Mr. Ahmed Noor Wako : Jina langu naitwa Ahmed Noor Wako. Umeandika huko. Sawasawa. Basi nafikiri mimi nitasema machache tu kwa sababu wengi wameongea. Mimi hapa kwanza mapendekezo tu ndio mimi nitasema hakuna haja mimi naongea mambo mengine.

Com. Lethome : Ndio sawa

Mr. Ahmed Noor Wako : Mimi nataka bank ya Kiislamu kwa sababu Serikali ya Kenya haitaki hata Waislamu. Lakini tunataka bank bila ribaa ambayo hata ikuje mpaka hapa kwetu ikiwezekana. Mimi najuwa vile wewe utaandika wewe ndio expert Bwana Sheikh.

Com. Lethome : Naam.

Mr. Ahmed Noor Wako : Ya pili, primary tunataka badala ya 8-4-4 irudishwe kama zamani kwa sababu hii ni kusumbua watoto na haiwezi kusaidia nataka ya kama zamani tu standard seven halafu form five form six halafu aendele mpaka University.

Ile ingine mimi nataka ingilia ni hapo kwa Parliament mimi nitasema kwa sababu mambo mingi watu wamesema sina haja ilikuwa mrefu. Parliament nafikiri mjumbe sisi raia ndio tunachagua. Lakini ukisikia upande hii ya Parliament baada kukaa kikao yao mara nane mbunge bado kufika kwa kikao huyo Speaker anaweza kusimamisha. Najua bunge lakini mkubwa wao ni sisi, sisi raia ndio anachagua. Sio Speaker alikuwa anachagua, Speaker aliona tu mjamua ameletwa na raia huko. Lakini mbunge inawezekana bila kufika miezi tano bila kukanyaga hata hii Garbatula kama ni ya Garba sehemu zingine yote.

Nikiongea tu kwa mfano hapa lakini hata sehemu zingine yote ni namna hiyo tu. Halafu mbunge bila kufika miezi tano hapa, count nane ndio nafukuzwa, kabla kufika miaka tano ikiwa mbunge anafanya makosa kama hiyo kutofika hata kwa citizens yake tunataka asimamishwe na Katiba kama hiyo iandikwe nyinyi ma-Commissioners mnajua vile mnaandika. Kabla kufika wakati huo. Hata ma-councillors pia namna hiyo.

Provincial administration tunataka ipigwe marufuku kwa sababu haiwezi kutusaidia hii ni kitu inangamiza sisi. Tusema kama tunachukua mfano hapa sisi tuko na Do ambaye yuko na ma-chief. Sasa mtu akikosana na chief hapa anaenda kwa Do. Chief huyu vile ameandikwa na Do ye ye ni sasa mambo yake hapa hawezo ogopa raia na

kimbia tu kwa Do na Do ukikimbia hapa ni kwa Dc. Sasa hawa isipokuwa huyu ni mdogo huyu ni katikati na yule mwininge mkubwa wa wote in chain of command ni kitu moja Chief akiwa anakuja kufanya makosa hapa anajua tu hiyo ili kuwa ni command ya Do, na Do akiamrisha Chief namna hiyo ikikuwa ni command ya Dc. Kwa hii watu wakishtakiwa hakuna namna wewe unaweza shtakia watu wote, ni mmoja tu.

Tunataka Koti ambayo ni independent ambayo tunashtaki watu wafanyakazi wa Serikali wote ambayo ipitishwe kwa Katiba mpya ili hawa hawahusika na administration halafu ikiwa Kotini na jengwa sisi tunashtaki hataikiwa ni mfanyi kazi yoyote wa Serikali ikiwa ana fanya makosa hatuwezi enda... Kama polisi tuseme tunashtaki kutoka hapa naenda kwa Ocpd mjamaa wakati wewe unaondoka hapa tu ameanza ku-contact yeye naongea na yeye halafu wewe ukikuja namna hii mambo yote inaharibiwa na yeye hataki kusikia wewe.

Na unapata gharama ikiwa sasa tena hawezi kuchukuwa ile maoni yako lakini tukipata Kotini independent kama hiyo nafikiri tunaweza kusaidiwa. Kwa sababu wale wanakaa hapa. Najua khabila ya Kenya arubaini na mbili mimi nataka ongeza hiyo pia. Wakati ambayo Katiba ilikuwa inatengenezwa bado wake watu wa Kenya, tunakaa namna gani pamoja. Bado ongea namna wale ambayo wanapigwa transfer hapa wanaletwa hapa nachukuwa wewe tu kama mnyama hawezi kuchukuwa kama binadamu. Kama ni mkubwa nafikiria tu mimi nitatajirika namnagani ili nirudi nijenge kwangu lakini mahali anasimamia yeye hajui sio khabila yao, lugha sio moja, dini sio moja, hakuna huruma yoyote ambaye iko nayo na huyu wananchi wanakaliwa kwa hivyo sisi tunataka ikiwa mambo kama hii sasa inaendelea Kotini kama hapa tunapata inaweza kutusaidia mambo yoyote kwa sababu wale ambayo wako hapa wote si watu wako na huruma na binadamu kwa sababu wewe saa hii ukipelekwa police station utastuka kwanza. Na hawo watu wanakaa hapa kwa sababu huduma yetu si ati wanakuja kushtuwa sisi namna hiyo. Ndio kwa ajili tunataka kuwekwe Koti.

Com. Lethome : Asante Ndugu.

Mr. Ahmed Noor Wako : Nitamaliza. Moja mimi naongea ni mambo ya transfer. Mfanyakazi wa Serikali anakuja makosa hapa anafanya makosa hapa na kosea watu hapa makosa kubwa anaweza fanya corruption anaiba mali ya watu halafu nyumae wakati unalalamikia juu yake zaidi inasemekana huyu atapigwa transfer mahali pengine ili aende aharibu mahali pengine kama hapa tu. Kama ni Headmaster wa shule hawa watoto yeye anakuja kusimamia hapa, watoto wanaanguka mtihani halafu nyumae mwalimu mwininge anakaa huko tuseme upande ya Dawa.

School inaendelea vizuri anapigwa transfer kutoka hapa anapelekwa kwa shule ambayo inaendelea vizuri na kwenda kuvunja ingine pia. Navunja mahali pengine. Mimi napendekeza ya kwamba mtu akifanya makosa yoyote asipigwe transfer aadhibiwe na makosa yake mahali ambao yeye anaishi bila kupeleka na anakwenda kuharibu watu

wengine tena. Kwa sababu hasara yake haiwezi kuwa mahali pamoja inakuwa mahali pengine. Do akifanya makosa hapa anapigwa transfer Embu nakwenda kuvunja huko. Baada ya huko anapelekwa Marsabit navunja huko. Kwa hivyo tunataka aadhibiwe watu wote mahali ambapo walifanya makosa bila kufanya namna hiyo. Iwekwe katika Katiba mpya sheria kama hiyo kwa sababu hawa watu wote bado kuongea walikuwa wananiwachia mimi najua.

Com. Lethome : Haya maliza Ahmed.

Mr. Ahmed Noor Wako : Haya mimi nitamaliza. Sheikh maramoja tu. Kumaliza kwangu sasa nitagusa tu mahali hapa sitaki hata mahali ambapo wale wamepitia sana lakini Duse. Hii sehemu hii ambayo ina husu zaidi ambayo mahali hii tumelalamikia, tumelalamikia lakini kitu ambacho kinatuhuzunisha kama unapitia huko watu wengi wame taja mahali hapo. Hapo ilikuwa na peanwa na hawa watu ambayo ni Provincial Administration wale ambao tunaongea mambo yao. Badala hawa watu Provincial Administration ambao inatuangamiza kiwango hiki ambaye wanapanga barabara hii kutoka hapa ambaye tuseme sehemu hii kitu ambaye mimi narudia zaidi barrier ambaye unaona hapa mpaka Nairobi hii yote inajua nawekwa kwa sababu ya Wariaa tu.

Hakuna khabla nyingine District ya Moyale District ya Isiolo ama hii ya Mandera barabara hii yote kwa sababu inangojea naenda Wariaa tu. Gari ile ambayo inaugonjwa kwa barabara wewe ukiona namna hii tu siku moja wewe natoka kwa barabara na kaa tu na Polisi hawa kama magari tuseme inabeba kahawa ama nini namna hii Polisi wanaangalia namna hii tu wanajua gari tofauti. Wakiona gari hii tuseme ya Wariaa ndio watu wanakimbilia gari yote inapigwa search inaangaliwa. Kwa hivyo hii sasa kubagua sisi katika Serikali ya Kenya hii Katiba mpya iwekwe na mara ingine mambo kama hii yote ifutiliwe mbali.

Mimi nitamaliza hapo asante sana.

Com. Lethome : Haya asante sana. Hussein Abdalla? Halafu Roba Galgalo yuko? Roba Galgalo hayuko? Adan Boso? Nuria Wario? Nuria? AaAa usimtafute kama hayuko? Usitafute wacha tu. Nuria Wario? Uko haya utafuata baada ya mzee.

Mr. Hussein Abdalla : Asalaam Aleykum ...[Arabic dialect]... Na simama hapa kupendekeza kwa niaba ya Waislamu ambaye wa sehemu hii nina karatasi nitapeana na sitazungumza sana lakini nataka kusema moja ama mawili.

Ya kwanza Katiba mpya napendekeza kwamba Katiba hii mpya ambayo itakayoundwa iwe ina hakikisha usawa kati ya wa Kenyan citizens bila kuwabagua kidini , kikabila, kigeographia ama kihistoria kwa sababu sisi hapa

tunabaguliwa saa ingine kidini, kigeographia labda watu wa sehemu hii zamani tulikuwa Nfd ama nini ama kihistoria fulani tusibaguliwe tupate haki.

Pili Katiba, sisi ni Waislamu na dini yetu inasheria yake sheria ya Kiislamu ambayo inatokana na kitabu cha mwenyezi Mungu tukufu kwa hivyo Katiba mpya itambue sheria Islamu ni sheria inatokana na mwenyezi Mungu wala si customary law ndogo ndogo ambazo zinaweza kugeuza huko na huko. Kwa hivyo mimi napendekeza ya kwamba Waislamu wa hukumiwe na sheria ya Kiislamu vile ambaye mwenyezi Mungu ...[Arabic dialect]... anataka.

Ya tatu Katiba mpya wakati itakapotengenezwa kifungo chochote katika hiki Katiba, kifungo yoyote katika Katiba mpya itakayotengenezwa isije ikahitilafiana na mafundisho ya dini ya Kiislamu kwa sababu italete shida na matatizo na ukosefu wa amani.

Kina mama na watoto wanapewa haki kamili katika Kiislamu. Haki ya urithi wanayo, haki ya heshima wamepewa, haki ya kuwa na mali wamepewa, haki ya binafsi yake amepewa, haki ya kijamii amepewa, kwa hivyo Uislamu inatetea haki ya kina mama mwaka elfu-moja-na-mia-nne iliopita na bado inaendelea kutetea naitatetea. Tunachotaka ni ...[Arabic dialect]... iundwe pamoja na ...[Arabic dialect]... ya Islamu ambaye italipwa na Serikali kutoka Treasury of the Government. Hii ndio itatetea jamii ya Kiislamu na Kadhi wetu kuanzia Chief Kadhi wapewe power ili waweze kulinda haki ya akina mama na watoto kulingana ma mafundisho ya Koran ...[Arabic dialect]... hakuna sheria ingine itawalinda.

Ya tano nasema, tuwe na presentation ya usawa katika Serikali ama katika Katiba ihakikishe ya kwamba tuwe na usawa kama ni katika mawaziri, kama ni katika key positions sisi Waislamu ambao tuko one third ya Kenya ionekane ya kwamba katika cheo kubwa kubwa katika Serikali na pahali ambaye key positions Waislamu waonekane ile population yetu itambulike kulingana na vile tunawakilishwa katika sehemu muhimu muhimu. Si leo hatuonekani tunakaa kama hapa sijui kama kitu imetupwa katika I don't know where.

Ya nne mimi nasema sisi sehemu hii ya Waislamu pamoja na pastrolists tumekuwa marginalized pamoja disabled watu walemvu yote tunataka affirmative action. Na hii mimi nataka Katiba hii ninapendekeza ya kwamba Katiba ipeane conducive supportive, peaceful environment ili sisi tuweze kuendelea na kuwashika wale ambao wametutangulia to catch up with the rest. Bila hiyo kama hatuna amani kama hatuna mazingara ambaye inaweza kukufanya wewe uendelee utaendelea vipi hata tukiimba hapa usiku na mchana Katiba ipeane hiyo.

Napendekeza ya kwamba election date ambaye leo imefuwa secret weapon ya Rais iondoke kabisa. Election date tarehe ya kura iweke katika Constitution tuambiwe ni tarehe fulani kura yetu tuje.

Ofisi ya Ombudsman iundwe Katiba ikubali ofisi kama hii iundwe ambayo mtu yoyote atadhulumiwa na ofisa yoyote ya Serikali aweze kwenda kushtaki pahali atapeleka malalamiko yake.

Na pia Constitutional Court Katiba ipatie provision Constitutional Court iundwe, ili wewe right yako ya Constitution ikiwa imekuwa violated by somebody unapata pahali pa kuenda kutetea kushtaki ili hiyo haki yako ambaye imekanya wa ulipwe.

Ya mwisho mimi nasema, amendment. Amendment isifanywe ya Katiba na bunge. Ikiwa inahitajika kufanya amendment ama marekebisheso fulani ndogo ndogo wananchi wahuishwe. Kifungo chochote ya Katiba ambacho inahusu dini ya mtu isifanyiwe marekebisheso kabisa. Haya machache napeana karatasi yangu ...*[Arabic dialect]...*

Com. Lethome : Nuria Wario halafu afuwatwe na Alkano Galgalo. Alkano yuko hapa? Hayuko. Roba Ali? Hayuko. Abdikarim Wako? Abdikarim Wako hayuko. Haya Nuria endelea.

Mama Nuria Wario : Asalaam Aleykum! *[inaudible]*

Com. Lethome : Haya endelea Mama Nuria.

Mama Nuria Wario : Waan ann seehuu issaaniin gaarbba kuun cuuf imbbetaanii

Translator : Mama anasema nyinyi nyote wa Garbatula munanifahamu.

